SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

UKURASA 3




## Wakazi nyumba Magomeni Kota kuanza kupewa funguo kesho


MAISHA
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili
MISHIKAKI YA KUCHOMA
MITINDO
GAUNI REFU
KATUNIKA
MNG'ARO WA HERENI
Unaoambatana na uso wenye tabasamu


UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Machi 27, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580897
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

### UCHAFUZI MTO MARA

# Wataalamu watoa ufafanuzi wa kina

**Mganga** Mkuu wa Serikali atoa angalizo matumizi maji, samaki... *Endelea ukurasa 2 ,4 na 17*



Mwonekano wa Mto Mara eneo la Daraja la Kirumi wilayani Tarime mkoani Mara. Picha ndogo: Komando wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Sajenti Cosmas Nyakaho, akichukua sampuli ya maji kwenye mto huo, wakati kamati ya kitaifa ilipokuwa inachunguza uchafuzi wa maji yake hivi karibuni. **PICHA: OMR**

## Auawa kwa risasi akidhaniwa mbwa

UKURASA 3

## Sababu 60% Watanzania kupata chanjo ya UVIKO-19

UKURASA 3

MICHEZO YANGA, AZAM ZATOLEANA MAPOVU UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

## UCHAFUZI MTO MARA:

# Wataalamu watoa ufafanuzi zaidi



**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya kitaifa iliyoundwa kuchunguza uchafuzi wa maji ya Mto Mara imetoa ufafanuzi kuhusu kiini cha tatizo hilo lililosababisha vifo vya samaki.

Kamati hiyo iliundwa Machi 12, mwaka huu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ikiwa na wajumbe 11 kutoka taasisi mbalimbali za serikali.

Kamati hiyo ilipewa siku saba kufanya kazi hiyo hadi Machi 19, mwaka huu ilipowasilisha ripoti ya uchunguzi wake kwa Waziri Jafo mjini Musoma.

Katika taarifa yake iliyowasilishwa mjini Musoma, Kamati ilibainisha njia kuu mbili zilizochafua maji ya Mto Mara; mosi ni kupitia mimea ya asili inayozalisha sumu na ya pili ni shughuli za kibinadamu zikijumuisha uwapo wa idadi kubwa ya mifugo inayozalisha ziada ya kinyesi katika maji hayo.

Hata hivyo, ripoti hiyo iliibua malalamiko kutoka kwa baadhi ya wadau wa haki, sheria, afya na mazingira, wakitilia shaka kiwango cha kinyesi na mkojo wa mifugo iliyotajwa na kamati hiyo kuwa sehemu ya kiini cha uchafuzi wa Mto Mara.

Kutokana na shaka hiyo, kamati hiyo jana ilikutana na waandishi wa habari jijini Dodoma na kutoa ufafanuzi wa kina namna ilivyofanya uchunguzi na ilichokibaini.

### UCHUNGUZI ULIVYOFANYIKA

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Prof. Samwel Manyele kutoka Idara ya Uhandisi wa Kemikali na Madini, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema uchunguzi wao ulianza kwa kuangalia jiografia ya mto huo kuanzia Kenya kupita Serengeti hadi eneo oevu la mto na jinsi unavyoingia kwenye Ziwa Victoria.

"Tulifanya vipimo vya papo kwa papo kwenye maeneo mbalimbali ya Mto Mara kwa ajili ya matokeo ya muda mfupi kujua tatizo lipo wapi kwa haraka haraka baadaye tukachukua sampuli za maji, samaki, mimea inayooza, udongo kutoka chini ya maji kwa ajili ya uchunguzi wa kina wa kimaabara," alisema.

Alibainisha kuwa mto huo katika eneo oevu juu kuna majani ambayo yamevamia mto na chini zaidi kuna kuna tope ambalo majani hayo yanaoza kwa muda mrefu.

"Tulifanya mikutano ya kila siku ya wajumbe wa kamati kupokea na kuchakata taarifa, tuliitisha taarifa mbalimbali kutoka kwenye taasisi za serikali zinazohusika kwa namna moja au nyingine lakini pia tulihitaji taarifa za magonjwa yaliyokuwa yametokea, yote haya yalichakatwa kwenye vikao.

"Tulifanya vikao usiku na mchana, tulifanya mahojiano na watumiaji wa Mto Mara ya ana kwa ana, wanakamati walizunguka maeneo yote ya mto na kuangalia vijiji vilivyo karibu, kuwakusanya wale wanakijiji na kuongea nao.

"Tulitumia dodoso maalumu lililotengenezwa na wanakamati, madodoso yalisambazwa na kujazwa tulipambanisha madodoso hayo kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wa madini wakubwa na wadogo," alisema.

Alisema walitembelea maeneo ya ardhi oevu kwa ukaribu kwa kutumia magari na boti.

"Kutokana na majani kutapakaa kwenye eneo hilo kuna maeneo yalikuwa hayafikiki, eneo hili ni kubwa kwa hiyo huwezi kwenda kwa boti wala kwa gari, baadaye tulitembelea maeneo hayo kwa kutumia ndege kutoka TANAPA, tuliomba watupitishe eneo la mto ili kuona uhalisia wa kuchafuka kwa maji.

"Tulitumia helkopta ili tushuke chini zaidi ili kuchukua picha na kuona kwa ukaribu, tulifanya hivyo, baadaye tulitumia drone na tuliituma kwenda ndani ya pori ikatuletee picha za maji, picha za majani na vinavyoendelea kule ili kuchakata hizo taarifa na kuona namna gani tutaweza kutambua kuchafuka kwa maji," alisema.

"Eneo hili linakaribiwa kuwa kilometa za mraba 423, upana kwenye eneo kama hili unakaribia kilometa 16, ni eneo kubwa," alisema.

### SAMPULI NA TAARIFA

Mwenyekiti huyo alisema walichukua sampuli kwa kutumia boti, magari, ndege na helkopta kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wakisaidiwa na makamanda wa jeshi hilo kuingia eneo oevu na kuchukua sampuli.

Alisema kwenye picha inaonyesha namna majani yanavyousonga mto na umebaki kuonekana kwenye maeneo machache na chini ya majani hayo kuna mto na majani yanaendelea kuoza mwaka hadi mwaka.

### MAJI MACHAFU

"Tukiwa kwenye boti inayokata maji, tunaangalia maji 'mbona hiki kitu cha ajabu, tunachukua picha na sampuli. Picha za kwenye ndege zinaonyesha maji ni meusi tii, na yanaendelea kutiririka kuelekea ziwani (Victoria), ni kama vile tumemwaga masizi mto wote, lakini tumeangalia majini ili kujua ni nini hasa.

"Tulishuka zaidi kwa helkopta hadi kwenye eneo na kuangalia eneo lingine maji yalivyokuwa yanatiririka na kweli tuliona kuna dalili ya vinyesi vya mifugo ambayo ilikuwa imepelekwa kwenye mto na hivyo kuacha kinyesi," alisema.

Alibainisha maji yanayotiririka yakiwa yamebeba kinyesi ni mbolea kwa ajili ya magugu maji na hivyo kuchangia kustawi zaidi.

"Kitendo cha kuyapa mbolea namna hii magugu maji kinafanya yakue kwa kasi na kujaa tena kuziba mto, maji kuwa meusi namna hii na kutiririka kwa kinyesi tunasema ni chanzo kikubwa cha kuchafuka kwa mto.

"Picha tulizopiga angani zinaonyesha mifugo bado ipo kwa uchache zaidi, bado kuna maeneo yanalishwa mifugo na sehemu ambayo wanalisha mifugo sasa hivi maji yapo salama," alisema.

Prof. Manyele alisema ukiufuata Mto Mara unapoelekea Ziwa Victoria kutoka kwenye Daraja la Kirumi, unapata kilometa 4.8 kutoka kwenye daraja kwenda ziwani.

Alifafanua kuwa kutoka darajani hadi eneo ambalo maji meusi yanaanzia ni kilometa 12, lakini eneo oevu linaendelea na shughuli za uchimbaji madini ziko mbali kwa kilometa 43 kutoka kwenye sehemu ambayo maji machafu yanaanzia.

"Kutiririka kwa maji machafu kwenda ziwani tulijaribu kufuatilia kasi ya weusi kuelekea ziwani, tulipanda boti kutoka darajani, tunayafuata maji hadi tunafika Musoma, dalili za kuanza kuchafuka maji zilikuwa zimeanza kusogea mpaka mjini, lakini maji meusi bado yalikuwa yanaelekea Ziwa Victoria, hayajafika," alisema.

"Eneo lenye maji machafu kwenye Mto Mara ni hizi kilometa 12. sampuli za udongo chini ya maji, tulichukua sampuli za kila aina, tumeainisha kwenye ripoti yetu," alisema.

Prof. Manyele alibainisha kuwa haikuwa kazi rahisi kwa kuwa eneo oevu ni kubwa, mto umezingirwa na magugu, sehemu zingine hazifikiki kwa boti na hivyo kulazimika kutumia helkopita.

Alisema katika kujiridhisha kama maji yana sumu au la, walichukua maji kwa ndani kabisa ambako hakufikiki na wala mifugo haifiki ili kujua kama kuna vitu vinadhuru binadamu au mifugo.

### KUWAPO MAFUTA

"Eneo kama lile fikiria ni kubwa lote linafanya uozo, vilevile tulipewa taarifa za awali na wenzetu wa bonde kwamba maji yalionekana yana utandu wa mafuta. Taarifa zao zilionyesha mafuta yapo mengi kwenye sampuli, kwenye maeneo mbalimbali, tukasema lazima tutambue huu utandu wa mafuta kwenye maji unatokana na nini? Ikiwezekana tujue hayo mafuta ni ya aina gani.

"Tulitakiwa tujue nini chanzo cha mafuta haya, tukaitisha taarifa za miamba iliyopo chini ya Mto Mara kutoka GST (Wakala wa Jiolojia Tanzania) wakatuletea taarifa,

INAENDELEA UK. 17

HABARI KITAIFA

# Sababu 60% kupewa chanjo ya UVIKO-19

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema endapo Watanzania asilimia 60 au 70 watachanja hapo ndipo watakuwa wameilinda jamii dhidi ya janga la ugonjwa wa UVIKO-19.

Katibu Mkuu Afya, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo juzi katika mahojiano na Nipashe iliyotaka kujua sababu ya kuwapo kwa mwitikio mdogo wa wananchi kupata chanjo hiyo, akijibu kuwa ni elimu kuhusu chanjo hizo.

Katika mahojiano hayo, Nipashe ilitaka kufahamu kwa nini hadi sasa ni asilimia 9.9 tu ya Watanzania waliochanjwa chanjo ya UVIKO-19.

"Tunatamani uchanjaji wa chanjo za UVIKO-19 upande angalau kwa asilimia 60 au 70 ya Watanzania wenye uhitaji wa kuchanja hapo tutakuwa tumeilinda jamii kupata ugonjwa huu. Chini ya hapo bado tutakuwa hatujailinda jamii," Prof. Makubi alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema Watanzania wanahitaji kupewa elimu zaidi kuhusu chanjo hizo zinazoendelea kutolewa na serikali.

"Watanzania wanahitaji kupewa elimu zaidi, wananchi hata ingelikuwa wewe kama kitu mwanzoni kilikuwa na mkanyanyiko mwingi -- wengine wanapinga, wengine wanaunga mkono. Kwa hiyo watu walichanganyikiwa kidogo, hili lazima tukubali," alibainisha Prof. Makubi.

Alisema kwa sasa kampeni zinaendelea kwenye mikoa na wilaya zikisimamiwa na viongozi na wengi wameelimika na wanaochanja wengi ni wa vijijini kulinganishwa na mijini.

"Kinachoendelea ni kuendelea kuelimisha umma faida za kuchanja na kuelimisha kuwa chanjo hizi ni salama," alisema.

Katibu Mkuu alisema wananchi wakiendelea kuelewa, mwitikio utakuwa mkubwa zaidi na hilo litasaidia kuwalinda.

"Ili tuweze kuendelea zaidi tunahitaji kuhamasisha kwa kutoa elimu kwa wananchi kwenye ngazi ya mitaa, vijiji ili wahamasike.

"Wizara tunawatumia viongozi wa mitaa, viongozi wa dini, watu maarufu na wanasiasa ili kuhamasisha wananchi kuchanja," alisema.

Ugonjwa wa UVIKO-19 uligundulika kwa mara ya kwanza Wuhan, China mwishoni mwa mwaka 2019. Tanzania iliripoti kupata mgonjwa wa kwanza Machi 16, 2020.

# Auawa kwa risasi akidhaniwa mbwa

**Na Waandishi Wetu**

MKAZI wa Kibosho Kindi katika Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Prosper Munishi (48), ameuawa kwa kupigwa risasi na ofisa wa wanyamapori aliyekuwa anatekeleza operesheni maalumu ya kuua mbwa wasio na wamiliki vijijini.

Taarifa zilizopatikana kutoka eneo la tukio na kuthibitishwa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Yahaya Mdogo, zilibainisha kuwa mauaji hayo yalifanyika Machi 24, mwaka huu.

Ilidaiwa kuwa Ofisa Wanyamapori, Honest Minja (35), aliyekuwa akiendesha operesheni hiyo, alimpiga risasi Munishi na kupoteza maisha.

"Mtuhumiwa tunamshikilia na uchunguzi unaendelea na ukikamilika atafikishwa mahakamani. Bunduki iliyotumika ni aina ya Shotgun yenye namba 31044 aina ya Greener,"alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Mdogo, mwili wa Munishi umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), ukisubiri taratibu zingine za uchunguzi wa kitabibu.

Baadhi ya mashuhuda waliozungumza na Nipashe, akiwamo Richard Mallya, walisema ofisa wanyamapori huyo alimfyatulia risasi Munishi ambaye ni fundi wa kuchomea vyuma katika eneo la Kibosho Kindi.

Mama wa marehemu, Auleria Paulo, akizungumzia kifo cha mwanae, alisema kuwa Munishi kabla ya kifo chake, alikuwa ametokea mjini Moshi kuchukua vifaa vya kazi yake.

"Alipofika nyumbani akaweka vifaa vyake na kuaga kwenda kumwona mtoto wa kaka yake. Mita chache baada ya kutoka nyumbani kwetu, alipotoka nje, ghafla nikasikia mlio ambao sio wa kawaida na nilipotoka, nilikuta ameshikilia moyo, huku damu zikichurizika.

"Hapo nje kulikuwapo na watu wasiojulikana, wakidai wapo kwenye operesheni ya kuua mbwa.

Baada ya kumpiga risasi walimchukua na kumweka kwenye gari na kuondoka naye.

"Mke wake aliamua kufuatilia Kibosho Hospitali na kaka yake akaenda Hospitali ya Mawenzi maana ilikuwa ni taharuki. Aliyefika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi alipata taarifa kwamba ameshafariki dunia," alisema.

Mkoani Katavi mwanaume aitwaye Laurent Buchumi (36), ameuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali shingoni na mke wake aliyetajwa kwa jina moja la Faidha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Ali Makame Hamad, alisema tukio hilo lilitokea Machi 24, mwaka huu katika kijiji cha Mchangani wilayani Tanganyika mkoani hapa.

Kamanda huyo alisema kuwa siku ya tukio, wawili hao walikuwa ndani ya chumba chao wanachoishi ndipo ulitokea ugomvi baina yao.

Kamanda Hamad alisema kuwa mume aliamua kutoka ndani ya chumba hicho kutokana na ugomvi huo na mtuhumiwa alimfuata na kumchoma na kitu hicho shingoni, kitendo kilichosababisha aanguke chini na kufariki dunia kisha mtuhumiwa kutokomea kusikojulikana.

Kamanda alisema mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi na juhudi za kumtafuta mtuhumiwa zinaendelea kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji.

Mbali na tukio hilo, Kamanda Hamadi pia alisema mwanamama Belta Fransisco (66) ameuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na watu wasiojulikana.

Alisema tukio hilo limeripotiwa katika Mtaa wa Ilembo, Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, ikidaiwa kuwa siku ya tukio marehemu alikuwa shambani kwake maeneo ya Ilembo ndipo wauaji hao walimfuata na kipiga kisha kutokomea kusikojulikana.

Kamanda alisema mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa ndugu kwa ajili ya mazishi huku juhudi za kuwatafuta watuhumiwa wa tukio hilo zinaendelea.

**•Imeandikwa na Mary Mosha (MOSHI) na Neema Hussein (KATAVI).**



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja akionyesha chemba ya maji safi iliyojengwa katika mradi wa maji wa Pugu-Gongo la Mboto, kwa wajumbe waKamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, walipotembelea mradi huo, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nyumba Magomeni Kota kuanza kukabidhiwa kesho

**Na Halfani Chusi**

WAKALA wa Majengo Tanzania (TBA) imefanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan Jumatano wakati wa uzinduzi wa nyumba za makazi za Magomeni Kota kuhusu wakazi kununua nyumba hizo kwa utaratibu wa mpangaji-mnunuzi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la nyumba za Magomeni Kota juzi mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Idara ya Miliki TBA, Said Mndeme, alikumbusha maelekezo hayo ya Rais Samia na wakala umeyapa kipaumbele na kuyafanyia kazi kwa haraka.

"Moja kubwa lililoelekezwa na Mheshimiwa Rais ni kuridhia wakazi wa nyumba hizi kuuziwa nyumba kwa utaratibu wa mpangaji-mnunuzi kwa kuzingatia hali zao za maisha kwa kurejesha gharama za nyumba pekee bila gharama ya thamani ya ardhi na miundombinu ya jumuiya ikiwamo maeneo ya korido, lifti na maeneo ya nje," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wakala umefanyia kazi maelekezo hayo kwa kufanya ukokotozi wa gharama hizo na kukamilisha na taratibu zinazofuata ni za kiserikali ikiwamo kupata vibali na baadaye gharama hizo kutolewa kwa wahusika.

Mndeme aliongeza kuwa utaratibu huo hautaathiri taratibu za makabidhiano na kuanza kwa matumizi ya nyumba hizo, akibainisha kuwa makabidhiano yataanza kesho kama ilivyopangwa na wengine kuanza kuhamia.

"Tayari tumeweka utaratibu mzuri wa kuhamia kwa wakazi wa hapa si kwa kupewa funguo. Kutakuwa taratibu za makabidhiano.

"Kuna fomu maalum zinazohusisha hali zote za nyumba na baada ya wakazi kuzikagua na kuridhika watasaini na maofisa wa TBA pia watasaini na watapewa pia barua za ofa zinazoonyesha wamepewa nyumba hizi kwa utaratibu wa mpangaji-mnunuzi.

"Ili kuhakikisha miundombinu ya nyumba hizo inakuwa vizuri muda wote, kutakuwa na wataalamu wa umeme na mabomba muda wote na wafanyakazi Idara ya Miliki ya TBA watakaokuwa wanasimamia nyumba hizi," alisema.

Mradi wa Magomeni Kota ulianza Oktoba Mosi, 2016 ukihusisha ujenzi wa majengo matano yenye ghorofa nane na tisa. Unatarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kutatua kero ya makazi kwa familia zaidi ya 600, zikijumuisha familia 544 zilizokuwa zikiishi katika eneo hilo awali.

# Uchafuzi wa Mto Mara unavyowatesa wakazi

## •Mganga Mkuu atoa angalizo kiafya

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

**KATIKA sehemu ya pili ya ripoti jana, kulikuwa na simulizi za vifo vya wavuvi watatu vilivyotokana na kunywa maji ya Mto Mara pamoja na waathirika walipoteza mifugo yao.Endelea na sehemu ya mwisho kujua undani wa mustakabali wake:**



Mvuvi akikatisha kwenye Mto Mara, hivi karibuni. Baadhi ya wavuvi waliripotiwa kuingia mtoni na kuchukua samaki waliokufa na kuelea baada ya mto huo kuchafuliwa. **PICHA: OMR**

### MTAZAMO LHRC, LEAT

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Chama cha Wanasheria wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) hawako nyuma katika ufuatiliaji wa suala hilo, wamependekeza mambo 12 kwa serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, anasema kituo hicho kwa kushirikiana na LEAT, walifuatilia kwa lengo la kujiridhisha kuhusu taarifa za uchafuzi wa Mto Mara, wakitembelea baadhi ya vijiji na vitongoji vilivyoathiriwa na uchafuzi huo.

Anayataja maeneo ambayo maofisa wao waliyatembelea kati ya Machi 17 na 20, mwaka huu kuwa ni pamoja na Makora, Burongo, Bisarwi Kati na Kwikoma yaliyoko Kata ya Manga wilayani Tarime.

Anna anasema katika ziara yao kwenye maeneo hayo ya waathirika wa uchafuzi huo, walibaini kuwapo taarifa za vifo vya mifugo ya wakazi wa maeneo hayo vinavyotokana na kunywa maji ya Bonde la Mto Mara yanayopita kwenye vijiji hivyo.

"Tulibaini kuwa katika kipindi cha kati ya mwaka 2018 na 2022, zaidi ya mifugo 800 ilikufa kutokana na kunywa maji yanayodhaniwa kuwa na sumu yanayopita katika Bonde la Mto Mara.

"Katika kipindi cha kati ya Machi Mosi na 15 mwaka huu, ng'ombe walioripotiwa kufa kutokana na kunywa maji ya mto huo ni 54. Taarifa hizo zilibainisha kuwa mifugo hukonda mithili ya kunyauka hatimaye kufa.

"Pale wakazi hao wanapochinja ng'ombe hao baada ya vifo hivyo, imethibitishwa na wenyeji kwamba nyama ilibadilika rangi na kuwa nyeusi, hivyo kutofaa kwa matumizi yoyote ya binadamu.

"Pia, mwaka 2020 na 2021 kulikuwapo na matukio ya kujirudia kwa wakazi wa vijiji hivyo kukumbwa na ugonjwa wa ngozi unaosababisha kuwashwa kwa ngozi na kujikuna kupita kiasi, ugonjwa huo ulipewa jina la 'Kwangua vocha'," Anna anasema.

Mkurugenzi Mtendaji wa LEAT, Dk. Rugemeleza Nshala, anawasilisha mapendekezo yao 12 kwa serikali, yakijumuisha utoaji wa haki ya kuishi na kufanya kazi katika mazingira yaliyo safi ambayo ni ya msingi na hivyo lazima iheshimiwe na wote ikiwamo watendaji wa serikali, taasisi au kampuni binafsi.

Dk. Nshala ambaye pia ni Rais mstaafu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), anasema hoja yao ya pili ni kukataliwa na kutupiliwa mbali kwa ripoti ya kamati ya kitaifa iliyoongozwa na Prof. Samuel Manyele kutokana na kile anachokiita kujawa upotoshaji juu ya sababu za uchafuzi wa Mto Mara.

"Makamu wa Rais ambaye ndiye waziri halisi wa mazingira nchini, aunde tume huru ya uchunguzi wa kitaalamu ikijumuisha wanamazingira wanaoaminika na weledi mkubwa kisayansi ndani na nje ya nchi," anasema.

Dk, Nshala anataja pendekezo lao la nne ni kuwasilishwa mara moja ripoti ya usafishaji wa maji machafu itolewayo kila mwezi ya mgodi wa dhahabu North Mara ambao mabwawa yake ya kuhifadhi maji machafu yako jirani na Mto Mara, eneo lililochafuliwa.

Anaitaja hoja yao ya tano ni kupimwa kiwango cha uchafuzi eneo husika ili kubaini kemikali na sumu zilizomo na la sita ni kuhojiwa bila vitisho wananchi wa maeneo husika pamoja na waathirika kujua kiwango cha athari.

Mkurugenzi huyo anasema mapendekezo mengine ni: Serikali ichukue jukumu la kusafisha eneo hilo lililochafuliwa na kudai fidia za gharama kutoka kwa mchafuzi kama inavyoelekezwa kwenye kanuni za mazingira; kutolewa haraka fidia na haki kwa waathirika na kuwajibishwa kwa watendaji wote wa serikali waliohusika na uchafuaji wa Mto Mara.

Mapendekezo mengine ni: Kuundwa upya kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutokana na kile ambacho Dk. Nshala anadai kushindwa kuchukua hatua stahiki za kupambana na uchafuzi wa mazingira katika eneo la Mto Mara; kutengwe bajeti kubwa ya kutoa elimu kukabiliana na uchafuzi wa mazingira nchini; na hatua madhubuti zichukuliwe na serikali kuwanusuru wakazi, mifugo na mazingira ya Mto Mara na Ziwa Victoria kwa ujumla kutokana na uwapo wa athari zinazoendelea kutokea maeneo hayo.

### MGANGA MFAWIDHI TARIME

Nipashe inatua mezani kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Tarime, Dk. Innocent Kweka, anayefafanua hatua walizochukua baada ya kupata taarifa za kuwapo uchafuzi wa Mto Mara unaotegemewa na wakazi wengi wiyalani hapa.

Dk. Kweka anasema wanafuatilia kwa kina kila mgonjwa anayefikishwa hospitalini hapo ili kujua kama ana ugonjwa uliosababishwa na kutumia maji ya mto huo yalipochafuliwa.

"Tunafuatilia kwa kina kujua kama ana shida kwenye ngozi au anaugua ugonjwa unaotokana na kutumia chakula kilichotoka kwenye maji ya Mto Mara ambao tumepewa taarifa umechafuliwa. Tumeweka tahadhari kubwa katika hilo.

"Tuna kitengo chetu cha magonjwa ya mlipuko na yale ya dharura. Pale ikitokea magonjwa ambayo si ya kawaida, kitengo chetu kiko tayari kwa lolote, lakini hadi sasa (jana saa 8:17 mchana), hatuna mgonjwa ambaye amefika hospitalini kutokana na madhara ya uchafuzi wa Mto Mara," alisema.

Alipoulizwa kuhusu vifo vya wavuvi waliohara na kutapika damu baada ya kunywa maji ya mto huo yalipochafuliwa miaka iliyopita, Dk. Kweka alisema:

"Kama kuna kesi ya aina hiyo itakuwa kwenye rekodi za hospitali, lakini mimi sijakutana nayo, pengine nilikuwa sijafika hapa."

### WALINZI WA MAZINGIRA

Dotto Mungo, Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Tarime, anapotakiwa kutaja hatua zilizochukuliwa kudhibiti uchafuzi wa mto huo, anasema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili watunze mazingira na kulinda vyanzo vya maji.

"Mwanzoni tulidhani kwamba athari zilizotokea za kuchafuliwa kwa Mto Mara zinatokana na Mgodi wa Dhahabu North Mara, lakini baada ya uchunguzi wa kamati ya kitaifa ikabainika kuwa hali hiyo haina uhusiano na mgodi huo, bali wananchi wenyewe. Ndiyo maana tunawapa elimu wajue kutunza mazingira," anasema.

Anarejea sheria zinazoongoza usimamizi wa mazingira nchini, zinaelekeza wananchi hawatakiwi kufanya shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji.

"Tunaamini kwamba elimu tunayoitoa kwa wananchi inaweza kusaidia athari zilizojitokeza katika Mto Mara zisijirudie tena," Mungo anasema.

### ANGALIZO LA SERIKALI

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, akizungumza na Nipashe jana kwa simu kuhusu suala hilo, aliwataka wananchi kutotumia maji ya Mto Mara kwa matumizi nyumbani.

"Kama tayari hao samaki wameshaathirika na wanakufa, kwa nini mtu ale hao samaki? Japokuwa sina uhakika ni sumu gani inayowaua, lakini tayari hii siyo dalili nzuri kuona kwamba samaki wanakufa.

"Tunachoshauri wananchi wasivue samaki kwa ajili ya kitoweo, wasioge kwenye hayo maji au kuyatumia kwa matumizi ya nyumbani, huu ndiyo ushauri," Dk. Sichalwe alionya.

### JAFO NA UTULIVU

Machi 21, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu uchafuzi wa mto huo, akiwataka wananchi kuepuka taharuki inayoendelea mitandaoni.

Waziri Jafo pia aliagiza timu ya wataalamu wa ofisi hiyo, Wizara ya Maji, Mifugo na Uvuvi kuchambua kwa kina na kuiweka wazi kwa umma kwa lugha ya Kiswahili ripoti ya uchunguzi wa uchafuzi wa mto huo.

Aliwataka Watanzania kuwa watulivu na kuepusha taharuki wakati serikali ikitimiza wajibu wake kwa kuwa azma ya serikali ni kulinda afya za wananchi wake, akisisitiza ripoti ya kamati ya kitaifa haikinzani na ya Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria.

"Nafahamu nimepitia mitandao nimeona kuna taharuki nyingi, niwaombe sana watu tuepuke taharuki wakati mwingine. Serikali inashughulikia haya mambo, tunatakiwa kushughulikia kwa hekima kubwa sana, sisi tuliunda timu tumepata taarifa na ripoti imepatikana," alisema.

Waziri huyo pia alikiri kuwa kwa sasa kuna tatizo kubwa la uchafuzi wa mazingira nchini, hasa magugu vamizi.

"Ukienda Ziwa Babati leo hii hali ya magugu vamizi imekuwa mbaya sana. Ukienda hata huo Mto Mara kwa mujibu wa picha nilizoona za wataalamu waliotoka 'site' (eneo la mradi) tuna hatari kubwa mbele ya safari kupoteza chanzo hiki muhimu. Changamoto ya magugu maji imekuwa kubwa sana nchini," alitahadharisha.

Waziri huyo aliongeza: "Zile picha za video wataalamu wakati wanaruka na ndege kuangalia Mto Mara ulivyo, lile eneo oevu lilivyovamiwa, inatupa shaka siku za usoni tusipofanya haraka.

"Ofisi yangu ndiyo imeunda hii timu (kamati ya kitaifa iliyochunguza uchafuzi wa Mto Mara) kwa kuwa kazi yake kubwa ni mazingira. Kwa hiyo, mtu mwenye maoni mbalimbali tunamkaribisha.

"Ofisi yangu ina jukumu la kuchukua kila kinachowezekana, jukumu letu kubwa ni kulinda mazingira, kulinda wananchi kwa nguvu zote. Kwa hiyo, mwenye maoni awasilishe hapa, sisi kazi yetu ni kupokea na kufanyia kazi," Dk. Jafo alihitimisha.

# COSTECH yazindua vipaumbele vya utafiti

**Na Mary Geofrey**

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imezindua vipaumbele vinne vya utafiti kwa mwaka 2021/23 hadi 2025/26, miongozo ya uanzishaji na uendeshaji wa kamati za kusimamia maadili ya utafiti na mwongozo wa kitaifa wa uanzishaji wa vigoda vya utafiti.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, alizindua vipaumbele hivyo jana mkoani Dar es Salaam, mchakato wake ukifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA).

Mkurugenzi wa COSTECH, Amos Nungu, alisema kwa kutumia Mwongozo wa Kitaifa wa Kusimamia Maadili ya Utafiti, tume imeratibu na kuwezesha kuandaa miongozo ya uanzishaji na uendeshaji wa Kamati za Kusimamia Maadili ya Utafiti katika zekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu kwa Tanzania Bara.

Alizitaja taasisi washiriki kuwa ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TALIRI), Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI).

Alisema tume inaendelea kuratibu na kuwezesha miongozo ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Kamati za Kusimamia Maadili ya Utafiti kwa taasisi za utafiti kwa upande wa Tanzania Zanzibar, katika sekta tajwa.

"Pia maboresho ya miongozo ya usimamizi wa utafiti katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na Ofisi za Makamu wa Pili wa Rais," alisema.

Alitaja maeneo yaliyozingatiwa kwenye vipaumbele vya kuanzisha mwongozo huo ni maendeleo ya maisha bora ya watu, kujenga uchumi wa viwanda ulio imara na wenye ushindani, utalii na urithi wa taifa.

Vingine ni maliasili endelevu na mazingira, masuala mtambuka ambayo yanajumuisha mabadiliko ya tabianchi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKAMA), ujasiriamali na matumizi ya rasilimali na bidhaa zinazotengenezwa nchini kwa maendeleo ya viwanda.

Naibu Waziri Kipanga, akizungumza kabla ya kuzindua vipaumbele hivyo, aliagiza utafiti wote utakaofanyika uwe umepitishwa katika kamati za maadili na kuidhinishwa na kupatiwa kibali na COSTECH kama taratibu zinavyotaka.

"Kutokana na umuhimu wa kamati hizi katika kukuza ubora wa utafiti, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kupitia uratibu wa COSTECH, itaendelea kuzijengea uwezo taasisi nyingine za kisekta zilizobakia kuhakikisha zinaanzisha kamati hizi za maadili," alisisitiza Kipanga.

Alisema serikali imeongeza bajeti ya COSTECH kutoka Sh. bilioni 3.8 hadi Sh. bilioni tisa ili kuongeza wigo wa vigoda vya utafiti nchini.

Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjobeing, aliahidi kufadhili Sh. bilioni 20 kwa ajili ya utafiti unaofanyika chini ya usimamizi wa COSTECH.

# Kesi waliojifanya maofisa usalama kuanza Aprili 4

**Na Kulwa Mzee**

KESI inayowakabili watu waliojifanya maofisa wa usalama wa taifa kwa kujitambulisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), inatarajiwa kuanza kusikilizwa ushahidi upande wa mashtaka Aprili 4, mwaka huu.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya, ilimuru hayo juzi wakati shauri hilo lilipotajwa tarehe ya kuanza kusikilizwa ushahidi, baada ya upelelezi kukamilika na washtakiwa kusomewa hoja za awali.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Joshua Kamalamo na Yahaya Kapalatu, ambao wanadaiwa kujitambulisha kwa DPP, Sylvester Mwakitalu na Naibu wake Joseph Pande kuwa ni maofisa wa usalama wa taifa.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai shauri lilipelekwa kwa ajili ya kupanga tarehe ya kuanza usikilizwaji baada ya upelelezi wa shauri hilo kukamilika na washtakiwa kusomewa hoja za awali.

Baada ya madai hayo, Hakimu Isaya aliahirisha kesi hiyo hadi Aprili 4, mwaka huu, kwa ajili ya kusikilizwa na washtakiwa wako nje kwa dhamana.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa walitenda makosa hayo Juni 12, mwaka 2021 katika ofisi za DPP zilizopo katika jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani, Dar es Salaam.

Ilidaiwa siku hiyo washtakiwa hao walijitambulisha kwa DPP Mwakitalu na DPP Pande kwamba wao ni maofisa kutoka usalama wa taifa, wakati sio kweli.




Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa duka jipya la kisasa la Tigo la Palm Village Mall, barabara ya Mwai Kibaki, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Pwani, Uthmaan Madati na Mkuu wa Kitengo cha Maduka na bidhaa za intaneti cha Tigo, Mkumbo Myonga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanafunzi aomba msaada wa matibabu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI Peter Makomba (19) (pichani), aliyekuwa akisoma kidato cha tatu Shule ya Sekondari Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga, ameshindwa kuendelea na masomo kutokana na maradhi ya mgongo yaliyomfanya apate ulemavu.

Alianza masomo kidato cha kwanza mwaka 2018, na mwaka jana (2021) ilipaswa awe amehitimu kidato cha nne, lakini kutokana na kupata maradhi ya mgongo hakuendelea na kuishia kidato cha tatu.

Baba wa mwanafunzi huyo, Emmanuel Makomba, akizungumza na Nipashe juzi nyumbani kwake, alisema mtoto wake alizaliwa bila ya kuwa na tatizo, lakini alipofika darasa la saba alianza kulalamika maumivu ya mgongo.

Alisema alipoingia kidato cha kwanza aliendelea kulalamika maumivu yanazidi, ndipo wakaanza kumpatia matibabu, lakini alipofika kidato cha tatu hali ikawa mbaya hadi akashindwa kutembea na kulazimika kuacha masomo ili aendelee na matibabu.

"Mtoto wangu kwa sasa hasomi tena shule alikomea kidato cha tatu baada ya kupata ugonjwa wa mgongo na kwa mujibu wa madaktari kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, mgongo wake umepinda mara tatu na ameshakuwa mlemavu tayari," alisema Makomba.

Alisema madaktari hao walimwambia ili mtoto wake apone anapaswa kupelekwa nchini India na itawagharimu Sh. milioni 40, lakini kutokana na kutokuwa na uwezo, ikabidi warudi nyumbani Shinyanga na kuanza kumtibu kwa njia za asili na kulipa Sh. 125,000 kila mwezi kwa dozi ya miezi sita.

"Awali mtoto wangu kabla ya kupata matibabu hata kidogo, hali yake ilikuwa mbaya zaidi alikuwa hawezi hata kutembea, lakini kwa sasa angalau anatembelea magongo na bado anaendelea na matibabu ya asili kwa sababu tulikosa fedha Sh. milioni 40 za kumpeleka nchini India kufanyiwa upasuaji," alieleza Makomba.

Naye mama mzazi wa mwanafunzi huyo, Joyce Ntumali, aliwaomba wadau, taasisi na mashirika mbalimbali, kumsaidia mtoto wao kiasi hicho cha fedha Sh. milioni 40, ili akapate matibabu nchini India ili aweze kurudi shule kuendelea na masomo na kutimiza ndoto zake.

Kwa upande wake mwanafunzi huyo, Peter Emmanuel Makomba, alisema yeye alianza kusikia mgongo unamuuma alipofika darasa la saba na wala hajui sababu ni nini, lakini alipofika kidato cha tatu hali yake ikawa mbaya zaidi na akaishiwa nguvu kwenye miguu na kushindwa kutembea tena.

Alisema kwa sasa baada ya kupata tiba asili angalau anatembea kidogo kwa kutumia magongo, lakini mgongo wake bado umepinda na hawezi kunyooka, na kuomba msaada wa matibabu kwa wasamalia wema ili aendelee na masomo na kutimiza ndoto zake za kuwa daktari.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ngokolo, Malale Masali, alikiri mwanafunzi huyo kusoma katika shule hiyo na kuishia kidato cha tatu baada ya kupata ugonjwa wa mgongo.

Alisema kwa taratibu za elimu, mwanafunzi huyo akipona anaweza tena kuendelea na masomo yake kwa kukariri darasa, kwa kuanzia pale alipoishia kidato cha



tatu, kwa wazazi wake kuandika barua pamoja na kuambatanisha nyaraka zote za matibabu.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo, aliwaomba watu binafsi, taasisi au mashirika watakaoguswa kumsaidia kupitia simu namba **0755912724, Emmanuel Makomba.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaokwamisha uwekezaji wachukuliwe hatua stahiki

**KWA** miaka kadhaa, serikali imekuwa ikiwavutia wawekezaji wa ndani na nje katika miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo itachochea ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini na kutatua tatizo la ajira miongoni mwa Watanzania, wakiwamo vijana.

Katika kuhakikisha azma hiyo inatimia, serikali ilianzisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa ajili ya kuratibu masuala hayo ikiwamo kutangaza fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali. Miongoni mwa sekta hizo ni madini, utalii, viwanda, kilimo, nishati, afya na elimu.

Licha ya kuanzisha TIC, serikali katika awamu tofauti imekuwa ikiteua mawaziri kwa ajili ya kusimamia uwekezaji ama kwa kuwa na wizara inayojitegemea kisekta au chini ya Rais au Ofisi ya Waziri Mkuu kulingana na mahitaji ya wakati husika.

Pamoja na kufanya hivyo, kulikuwapo malalamiko kwamba kumekuwa na umangimeza katika kuwawezesha watu wanaotaka kuwekeza. Baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa yakilalamikiwa ni upatikanaji wa vibali vya kazi na ukaazi, tathmini ya mazingira, upatikanaji ardhi na leseni kwa ajili ya kufanya shughuli ambayo mwekezaji amekusudia kuwekeza.

Kutokana na vikwazo hivyo, serikali iliamua kuweka vitengo vya taasisi zote zinazohusika na utoaji vibali na leseni kwa wawekezaji katika ofisi za TIC. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa kuwaondolea kero na usumbufu kama vile rushwa na kutumia muda mrefu katika kufanikisha uwekezaji.

Kwa mantiki hiyo, shughuli zote kama vile uhamiaji, maombi ya leseni na kufungua kampuni zilikuwa zikifanywa ndani ya ofisi za TIC hatua ambayo ilifanikisha kupunguza muda wa wawekezaji watarajiwa katika kupata nyaraka zinazotakiwa.

Pamoja na kuwapo kwa unafuu huo, hivi karibuni yamejitokeza madai kuwa bado kuna mambo ambayo yanakwamisha azma hiyo ya serikali kutokana na kuwapo baadhi ya watumishi katika ofisi za serikali wanaowahujumu wawekezaji.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, wakati wa mkutano wa kutia saini mkataba wa miaka mitano wa ushirikiano wa kukuza biashara kati ya Tanzania na India, aliibua jambo hilo ambalo linarudisha nyuma mpango wa serikali wa kuvutia uwekezaji katika sekta mbalimbali na hatimaye kukuza uchumi na kupunguza umaskini.


Bila kumung'unya maneno, Naibu Waziri Kigahe alisema anashangazwa na kuwapo kwa vitendo hivyo wakati serikali iliweka wazi kuwa mtu anapofika na kuwasilisha maombi TIC, anatakiwa awe amehudumiwa ndani ya siku saba. Hakuishia hapo bali aliweka wazi kwamba serikali italishughulikia suala hilo na kuwachukulia hatua wale wote wanaokwamisha juhudi hizo za serikali.

Pia alisema serikali itaendelea kutoa elimu kwa wawekezaji ili wajue taratibu wanazopaswa kuzifuata kutokana na kuwapo kwa watu wasio sahihi ambao wamekuwa wakisababisha serikali kulaumiwa kuwa inawakwamisha. Hatua hiyo alisema itasaidia kupunguza watu wanaojifanya wataalamu (vishoka) ambao wamekuwa sababu ya wawekezaji kuzungushwa kwa sababu ya kutojua taratibu.

Hatua ambayo serikali imeamua kuchukua inapaswa kupongezwa kwa sababu itachochea uwekezaji na kuitangaza Tanzania kuwa ina mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji, ikiwamo kutokuwapo kwa ukiritimba katika utoaji vibali na leseni kwa wale wanaokidhi vigezo.

Kwa upande wa watumishi ambao wanachafua taswira nzuri ya serikali, hawana budi kuchukuliwa hatua kwa sababu wanaojiingiza katika vitendo kama hivyo hawana tofauti na watu wanaohujumu uchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Usafi katika biashara ya mamalishe ni muhimu



Na Sabato Kasika

**MOJA** ya mambo ambayo mamalishe na babalishe wamekuwa wakihimizwa na watu wa afya, ni kuzingatia usafi wakati wote wanapofanya biashara hiyo kwa ajili ya usalama wa afya za wateja wao.

Suala la uvaaji wa kofia ni moja ya mambo ambayo watu wa afya husisitiza kwa kila mmoja wao wawapo katika biashara hiyo, ili kuepuka uwezekano wa nywele kudondokea kwenye vyakula.

Pamoja na msisitizo huo, bado wapo baadhi yao ambao hawazingatii hilo, badala yake hufanya biashara hiyo wakipika vyakula na kuwahudumia wateja bila kuvaa kofia kama wanavyoelekezwa.

Kimsingi, suala la usafi katika biashara hiyo ni la muhimu katika uandaaji wa vyakula, hivyo ingekuwa ni vyema wahusika wakatambua hilo na kuchukua hatua ambazo zinaelekezwa na wataalam wa afya.

Yako maeneo mkoani Dar es Salaam ambako biashara hiyo imeshamiri, lakini baadhi ya wanaofanya biashara hiyo hawazingatii uvaaji wa kofia wala 'eproni' kama sehemu ya usafi wawapo kazini kwao.

Kama watakuwa hawajui umuhimu wa kuvaa kofia wanapokuwa katika biashara hizo, basi ninadhani mamlaka husika zina wajibu wa kutoa elimu kuhusu usafi huo ili watambue na kuchukua hatua.

Binafsi ninaamini kwamba, suala la kuvaa kofia si kwa ajili ya afya za wateja tu bali hata wao wenyewe, kwani wanaweza kuhatarisha afya zao kwa kujua au bila kujua. Kwa hiyo ingekuwa vyema wakachukua hatua zinazostahili.

Kwa mfano, mamalishe au babalishe anaweza kuandaa chakula bila kuvaa kofia, nywele zikadondokea katika chakula ambacho hata mwenyewe anaweza kukitumia, na hivyo kujidhuru mwenyewe.

> **Kama wanafanya hivyo, kwa sababu ya ukosefu wa sehemu ya kutunzia takataka, basi ingekuwa ni vizuri kama mamlaka husika zitaliona tatizo hilo na kuwatengea maeneo rasmi ya biashara.**

Haipendezi mamalishe kusuka rasta na kuziachia bila kuvaa kofia kisha akaenda kuwahudumia wateja, bali anatakiwa aangalie usalama wa afya yake na ya wateja wake kama njia mojawapo ya kuvutia wateja zaidi.

Suala la kulinda afya zao ninaamini liko ndani ya uwezo wao, hivyo ingependeza kama watazingatia usafi ikiwamo pia wa mazingira wanayofanyia biashara zao kwa kutomwaga ovyo mabaki ya chakula.

Imekuwa kawaida kukuta baadhi ya mamalishe na babalishe wakimwaga maji waliyooshea vyombo vyao yakiwa na mabaki ya vyakula, katika mitaro au eneo lolote la wazi, hali ambayo kiafya si salama.

Kama wanafanya hivyo, kwa sababu ya ukosefu wa sehemu ya kutunzia takataka, basi ingekuwa ni vizuri kama mamlaka husika zitaliona tatizo hilo na kuwatengea maeneo rasmi ya biashara.

Ni vyema kila halmashauri ikaangalia uwezekano wa kuwasaidia wafanyabiashara hao ili waboreshe huduma zao badala ya kuendelea kuzifanyia katika maeneo ambayo si rasmi bila kuzingetia usafi.

Katika hali hiyo ya kuwaacha kama walivyo, inasababisha wamwagwe mtaroni au barabarani bila kujali kwamba huo ni uchafuzi wa mazingira. Lakini pia suala la wao kuzingatia usafi kwenye biashara zao ni la msingi.

Mamalishe na babalishe wamejipatia umaarufu katika biashara yao, kutokana na kuuza vyakula kwa bei ya chini inayoendana na uwezo wa kiuchumi wa wateja wao wa kutomudu kununua chakula cha bei ya juu.

Hivyo, kwa kuwa biashara hiyo imeshamiri maeneo mbalimbali nchini na hasa mijini, na kuongeza ajira inayowafanya wajikimu kimaisha, ni vyema wakaiboresha kwa kuzingatia usafi ili kuvutia wateja zaidi.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Kongole TotalErnergies kuonyesha njia nishati jadidifu, wengine waige



Na Pascal Mayalla

**Asilimia 70 ya nishati yote Tanzania, hutumika kwa kupikia, ikifuatiwa na mafuta na umeme. Nishati kubwa inayoongoza kutumika kupikia ni tungamotaka (biomass).**

WIKI hii imeanza kwa uzinduzi wa kituo cha kwanza cha mafuta nchini kutumia nishati jadidifu. Kituo hicho kinatumia nishati ya jua kuendesha kila kitu, hivyo kupunguza matumizi ya umeme na kutumia umeme safi na rafiki wa mazingira.

Kituo kilichozinduliwa ni cha kampuni ya mafuta ya TotalEnergies, mtaa wa Samora jijini Dar es Salaam na uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati, January Makamba.

Mkurugenzi Mkuu wa TotalEnergies Marketing Tanzania, Ltd, Jean-Francois Schoepp, wakati wa uzinduzi huo, alisema kati ya vituo zaidi ya 100 vya mafuta vya TotalEnergies nchini, 24 tayari vimeshafungwa umeme jua. Akaongeza kwamba kufikia mwakani, vituo vyote vya kampuni hiyo vitatumia umeme jua.

Uamuzi wa kampuni kutumia nishati jadidifu ni wa busara na wa kimaendeleo, hivyo unafaa kupigiwa mfano na kampuni zingine.

Busara za uamuzi huo ni kuukubali ukweli wa hali halisi ya umeme wetu kwenye gridi ya taifa ya megawati 1,600 kwa nchi yenye watu milioni 60 hautoshi.

Kwa mantiki hiyo, matumizi yoyote ya nishati jadidifu kwa mtu yeyote, taasisi, kampuni au ofisi yoyote ni muhimu na yatalisaidia taifa kwa kutoa fursa kwa wengine kutumia umeme wa gridi ya taifa na kulipunguzia taifa mzigo.

Waziri Makamba, katika uzinduzi huo, aliipongeza TotalEnergies kwa kuzindua kituo cha kwanza kinachoendeshwa na nishati ya umeme jua na kusema matumizi ya umeme jua, umeme wa upepo, umeme wa joto ardhi na mwingine wowote jadidifu, ndiko dunia inakokwenda. Kwa hiyo TotalEnergies wanastahili pongezi kwa kuonyesha njia, hivyo wengine wafuate.

Waziri Makamba alisema Tanzania chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kufanya mapinduzi makubwa ya nishati kwa kuifanya nishati ya kupikia, kupatikana kwa wingi na kwa urahisi zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki,

Kati na Kusini. Asilimia 70 ya nishati yote Tanzania, hutumika kwa kupikia, ikifuatiwa na mafuta na umeme. Nishati kubwa inayoongoza kutumika kupikia ni tungamotaka (biomass).

Pamoja na hayo, katika haya mambo ya nishati ya mafuta na gesi inayoagizwa nje ya nchi, kuna jambo moja kubwa ambalo silielewi. Baadhi ya nchi jirani, zinaagiza gesi, mafuta ya taa, petroli na dizeli, kupitia bandari ya Dar es Salaam.

Nishati hiyo inayoagizwa na nchi hizo na kupita nchini mwetu, inasombwa kwa malori ya mafuta mpaka nchini mwao lakini cha ajabu nchi hizo huuza mafuta kwa bei nafuu kuliko Tanzania. Wakazi wote wa mikoa ya mipakani, hujikuta wananunua mafuta ya jirani zetu kwa bei nafuu kuliko mafuta yetu.

Enzi za Mwalimu, baadhi ya bidhaa muhimu zikiwamo mbegu, mbolea na pembejeo za kilimo, zilifanywa bei nafuu kuliko hata bei halisi kwa kupewa ruzuku ya serikali ili wananchi wamudu gharama. Kuna wakati wa uhaba wa maji, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilikuwa linatumia gharama kubwa kuzalisha umeme wa gesi na mafuta na kuuza kwa bei ndogo kama ya umeme wa maji ili kutowabebesha wananchi mzigo wa gharama.

Hali ya nishati nchini si nzuri. Watu 22,000 wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na magonjwa ya upumuaji yanayosababishwa na moshi wa kupikia kwa kuni na mkaa.

Kutokana na hali hiyo, kipaumbele cha kwanza kwenye sekta ya nishati kiwe kuhakikisha gesi inapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu na inafika kila mahali. Hatua hiyo itapunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Kama TANESCO iliuza umeme kwa bei ya chini na enzi za JPM gharama za kuunganishwa umeme wa REA zilikuwa Sh. 27,000 tu na kushuhudia umeme ukifungwa mpaka kwenye vibanda vya nyasi, je, kuna ubaya gani serikali ya Mama Samia, ikaondoa kodi zote kwenye gezi ikiwamo VAT kwenye majiko ya gesi na gesi ya kupikia?

Kwa kufanya hivyo, maisha ya Watanzania 22,000 wanaokufa kila mwaka kwa matatizo yanayosababishwa na matumizi ya kuni na mkaa, yangeokolewa kwa matumizi ya gesi na umeme.

**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania tusijisahau tukarudi tulikotoka



Na Joseph Kulangwa

**Nilijiuliza kwa nini kinamama hawa wanapagawa hivi kwa kupata maji ya bomba? Leo zaidi ya miaka 60 ya Uhuru kinamama zetu wanafurahia hivi utadhani leo ni mwaka 1961 kwamba mkoloni leo kaondoka!**

NAFIKIRIA zamani zile tunakua, sikumbuki kuwapo shida sana hususan kwetu watoto kwani tuliishi na wazazi wetu vizuri bila kutambua kuwapo adha za hapa na pale na changamoto kwa familia.

Nakumbuka wakati nakua, nilikuwa namwona mama na dada zangu wakienda bondeni na mitungi na vibuyu na kurudi na maji ambayo tulikunywa bila kuchemsha na mengine wakipikia chakula.

Sikupata kuona hata siku moja nguo zikifuliwa nyumbani au mtu akiogea nyumbani. Kila aliyetaka kuoga au kufua, aliteremka bondeni mtoni na kufua na kuoga huko huko. Huo ndio ulikuwa utaratibu.

Nilipokua kidogo na kutambua hili na lile, siku moja nikaenda na kaka zangu bondeni kuoga, ndipo nikabaini kuwa kumbe wanawake na wanaume walitengwa na kichaka kilichokuwa mtoni na kila upande ulifanya yake na kuondoka.

Hakukuwa na tabia mbaya ya watu kuingiliana kama yanayofanyika leo hii kwani kosa hilo lingesababisha kesi nyingi za ubakaji na udhalilishaji mwingine wa kijinsia.

Jinsi miaka ilivyosonga mbele, tukahamia mjini ambako hakukuwa na mabonde na vijito vya watu kuoga na kufua bali kulikuwa na mabomba ya maji tiririka. Kwangu mimi ulikuwa mshangao, lakini nikazoea kidogo kidogo.

Nikaambiwa kuwa maji hayo yanatoka ziwani lakini yanapitia kwenye matangi kusafishwa na kisha kuingia kwenye mabomba ambapo hata kunywa tulikunywa hivyo hivyo kutoka kwenye bomba, hatukusikia madhara yoyote.

Lakini kubwa lililonishangaza zaidi ni kwamba kulikuwa na mabomba ambamo tulipenyeza sarafu na maji kutoka. Hizo ni enzi za Mwalimu Julius Nyerere.

Ghafla maisha yaliposonga zaidi mbele, mabomba hayo ya kuingiza sarafu yakatoweka, yakaja haya ya mita. Hata mitaa enzi hizo mingi ilikuwa na lami, lakini nayo katikati hapa ikatoweka.

Sasa kinachonishangaza mimi hivi karibuni nikiangalia luninga, nikamwona Chifu Hangaya akifungua nadhani huduma ya maji bila shaka Chalinze, nikaona jinsi kinamama walivyofurahi, utadhani nchi inazaliwa.

Nilijiuliza kwa nini kinamama hawa wanapagawa hivi kwa kupata maji ya bomba? Leo zaidi ya miaka 60 ya Uhuru kinamama zetu wanafurahia hivi utadhani leo ni mwaka 1961 kwamba mkoloni leo kaondoka!

Mi nadhani kuna mahali tumekwama kujitambua kwamba ni kwa nini zamani mambo mengi yalikuwa mazuri lakini jinsi tunavyosonga mbele yanaharibika na viongozi baadhi yao wanafunga macho?

Hivi wakati ule mabomba yanatoa maji kwa kuchomeka tu sarafu kama ilivyokuwa kwenye muziki kwamba unaweka pesa muziki unapigwa, au unaingiza sarafu soda ya kopo inadondoka, au kwenye ATM ya pesa au ya maziwa huko Uchagani.

Teknolojia hiyo kumbe ilikuwapo miaka mingi, lakini kwa uzembe wetu na sababu zetu tukaiua na sasa tunashangilia maji kutoka kwenye bomba la kawaida, tena umbali mrefu kutoka majumbani ikilinganishwa na zamani ambao ulikuwa mrefu zaidi.

Maendeleo anayoyasimia Chifu Hangaya leo, si ajabu baada ya miaka kadhaa tukayachezea na kujikuta tunaanza upya kama tunavyofanya hivi sasa. Tulikuwa na vitu vizuri lakini leo utadhani hatukupata kuwa navyo.

Watanzania imekuwa ni kawaida yetu kuchukulia mambo kimazoea na kutotafakari kuwa huko mbele yatakuwaje na kujikuta tunafuja maendeleo na kulaumiana, lakini ni kutokana na uzembe wetu.

Nani hakumbuki kuwa wakati ule tunasoma, elimu ilikuwa bure kuanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu? Leo akija mtu akasema tunatoa elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu itakuwa sawa na nchi kuanza upya.

Nakumbuka enzi hizo wazazi walichokuwa wanajali ni kununua sare tu, kwa sababu hata masuala ya nauli hayakuwapo, tulikanyaga kwa mguu kutoka nyumbani hadi shuleni na kurudi, huku tukipata kifungua kinywa cha uji au bulga. Madaftari, penseli na peni bure.

Chuo kikuu hakukuwa na malipo zaidi ya kulipwa posho kila mwisho wa mwezi huku chakula tukifakamia bure, kuanzia asubuhi, mchana mpaka usiku, kumbuka na jioni kukiwa na chai tena ya maziwa au maziwa yenyewe. Tumetoka mbali, twendako pia ni mbali.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Mrema ameshafunga ndoa yaliyoko mitandaoni ni wivu



Na Thobias Mwanakatwe

WIKI hii Mwenyekiti wa Tanzania Labour Party (TLP), Augustine Mrema, alijadiliwa sana kwenye mitandao ya kijamii baada ya kutangaza kuwa anataka kuoa binti mdogo na mweupe.

Wabongo kama kawaida yao, baada ya kusikia taarifa hizo, walianza kujadili ndoa ya Mrema huku wengine wakiweka hata picha za msichana waliyedai anataka kumuoa ambazo hazikuwa za kweli.

Katika mijadala, baadhi walifikia hatua ya kuanza kumchonganisha Mrema na familia yake kwamba watoto wake walikuwa wamekataa baba yao kuoa mwanamke mwingine. Mrema alichukua uamuzi wa kuoa baada ya mke wake, Rose, kufariki dunia Septemba, mwaka jana.

Watu hao ambao nawaita ni wanafiki, kwenye mitandao ya kijamii waliendelea kusema kama Mrema atafunga ndoa katika kipindi hiki cha Kwaresma, atakuwa amekiuka taratibu za Kanisa Katoliki ambazo kwa mujibu wa wao, hairuhusiwi.

Mijadala yote hiyo ilikuwa ikiendelea hata kabla ndoa haijafungwa lakini mzee Mrema hakukatishwa tamaa, akaendelea na maandalizi ya harusi yake kama kawaida.

Ilipofika Alhamisi, Machi 24, 2022, Mrema na mke wake mtarajiwa, Doreen Kimbi, wakajitokeza katika Kanisa Katoliki Parokia ya Uomboni, wakafunga ndoa kama kawaida, hivyo kuwaacha midomo wazi waliokuwa wakijadili suala hilo.

Kutokana na ndoa hiyo, waliokuwa wakijadili na kufukunyua mambo, wakabaki kama wamepigwa na kitu kizito kichwani kwa sababu picha ya mwanamke waliyekuwa wakimweka mitandaoni kwamba ndiye anaolewa na Mrema, ikawa tofauti na aliyejitokeza kanisani.

Baada ya ndoa kufungwa tu, wakaanza kuzua jambo jipya kwamba eti huyo mwanamke alikwishaolewa na mwanamume fulani na akaachika. Wakaenda mbali kwa kusambaza picha za mwanamke huyo akiwa na mwanamume ambaye walidai ni mume wake wa zamani.

Pia wakazusha kuwa mwanamke huyo amefuata hela kwa Mrema na kwamba mzee huyo kashamkabidhi hata kadi za benki. Lakini yote hayo Mrema akayapuuza na kuyaona ni uzushi tu.

Hivi sasa mzee Mrema anaendelea kula bata na mke wake. Waliokuwa wakishobokea ndoa hiyo kwa kuzusha kila jambo, wamebaki na umbeya wao mifukoni.

Uzushi ulioenezwa kabla na baada ya Mrema kufunga ndoa, hauleti afya kwa jamii ya kitanzania ambayo inatambua ustaarabu. Sote tunatambua kuwa Mrema ambaye ameshika nyadhifa mbalimbali za uongozi hapa nchini, ikiwamo ya Naibu Waziri Mkuu, ni mtu makini.

Kwa anayemjua Mrema, hawezi kukurupuka na kuanza kumshutumu kuwa eti ameoa mke wa mtu. Wako wanaoweza kufanya hivyo lakini si kwa Mrema. Pengine waliokuwa wakizusha yote hayo kabla na hata baada ya kufungwa ndoa, walidhani watamdhoofisha Mrema kisiasa na ndoa yake huku wakisahau kuwa walichokuwa wakikifanya ni kuzidi kumpaisha kwa umaarufu.

Nilifurahishwa na Mrema alivyowapa 'dongo' kiaina waliokuwa wakiendelea kuijadili ndoa yake pale alisema wanaoendelea kueneza uzushi na upotoshaji kwenye mitandao ya kijamii, wanapoteza muda wao na vijiba vyao vya roho.

Mrema alisema uvumi wa mambo yote hayo unatokana na kwamba watu hawajazoea mtu akipendwa kwa dhati na mtu mwingine bali wamezoea rushwa wanahonga watu, wananunua watu, kwa hiyo wanafikiri kila mtu ananunulika.

Mrema awali alikwisha weka wazi kuwa alifuata taratibu zote zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kulipa mahari na taratibu nyingine za kimila zinazostahili. Alisema sababu zilizomfanya aoe tena ni baada ya mke wake kufariki dunia na kumwacha katika mazingira magumu, hivyo alimwomba Mungu amsaidie ili apate msaidizi mwingine.

Sasa kama Doreen na Mrema walikaa pamoja wakajadiliana na kukubaliana wafunge ndoa wawe mwili mmoja, wewe ni nani hadi uanze kutokwa na mishipa kuzusha umbeya kwenye mitandao ya kijamii. Ona sasa aibu imekushika.

Ifike wakati tunaotumia mitandao ya kijamii tuwe wazalendo wa kweli kwa kuitumia vizuri. Tusipende kuzusha mambo yasiyo ya kweli ambayo hayana faida zaidi ya kuvuna dhambi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia baruapepe: mwanakatwe2005@yahoo.com au 0692-276999**

## DARASA LA NDOA

# UWAPO WAKO NYUMBANI UNALETA AMANI NA FURAHA KWA FAMILIA?



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

AMANI na upendo ndani ya familia ni vitu vya muhimu katika kudumisha na kustawisha ndoa. Wenye jukumu la kusababisha haya yatokee ni wanandoa wenyewe na hapo ndipo thamani ya mtu inapoonekana.

Kama ambavyo nilieleza katika makala za awali, thamani ya mtu haipimwi kwa uwapo wake bali kwa yale anayotenda. Ili mtu kujua thamani yake ndani ya familia, anapaswa kufanya tathmini binafsi (self-assessment).

Hiyo itamwezesha kujua kama uwapo wake umeongeza au umepoteza thamani ya mwenzi wake.

Jambo la msingi la kulitambua ni kwamba kama mtu uwapo wake hauambatani na matendo mema kwa familia yake, anapoteza umuhimu, mvuto na mguso (positive significance) katika familia.

Kwa maana hiyo, inawezekana mtu huyo amekaa katika nafasi ya mtu mwingine ambaye angeweza kuwa na mguso huo.

Katika jamii kuna watu wa aina mbili; watu wenye kuongeza thamani katika maisha ya watu wengine (value adders) na wanyonyaji (parasites) ambao hawaongezi thamani katika maisha ya wengine. Watu wa aina hii mara nyingi huwa ni wepesi wa kulaumu. Kinachowafanya waendelee kuwapo katika maeneo yao ya kazi ni unafiki na jitihada katika kufanya majungu.

**Kwa wanandoa, swali la msingi la kujiuliza ni je uwapo uwapo au kutokuwapo nyumbani kuna mguso au athari yoyote? Ukifa utakumbukwa kwa jambo lipi? Robin Sharma, mwandishi wa kitabu kiitwacho, "When you die who will cry?" anauliza swali hili zito ambalo linahitaji mtu kufanya tafakuri ya kina.**

Kwa wanandoa, swali la msingi la kujiuliza ni je uwapo au kutokuwapo nyumbani kuna mguso au athari yoyote? Ukifa utakumbukwa kwa jambo lipi? Robin Sharma, mwandishi wa kitabu kiitwacho, "When you die who will cry?" anauliza swali hili zito ambalo linahitaji mtu kufanya tafakuri ya kina.

Mwandishi kutokana na maswali hayo, anajaribu kuifikirisha jamii kwamba mtu anapopumua haimaanishi kuwa anaishi; kwamba anapokwenda huku na kule, haimanishi kuwa anapiga hatua mbele au anapiga sana kelele haimaanishi kuwa watu wamemsikia.

Kwa mantiki hiyo, maisha si suala la uwapo wa mtu bali hupimwa kwa mguso unaotokana na matendo mema.

Ni muhimu mtu kuwa na utambulisho mzuri kwa watu kutokana na kila jambo analolitenda.

Aonyeshe upekee wake kwa kutenda mema ili akumbukwe na aendelee kuishi katika mioyo ya watu kwa kuwa thamani yake imefungamanishwa katika upekee huo.

Mume na mke ni muhimu waonyeshe upekee wao katika ndoa kwa kuwa ndoa ni wajibu. Kwa mantiki hiyo, wanandoa watambue nafasi na wajibu wao.

Furaha na mafanikio katika ndoa vitakuwapo pale kila mwanandoa atakapotimiza wajibu wake na kumtanguliza Mungu.

Ni muhimu wanandoa wajifunze kuishi maisha yao ili kutunza amani na utulivu.

Wanandoa wanapaswa kuishi maisha yenye mguso, mvuto na kufurahiana.

Hali hii haiji kimiujiza bali hutengenezwa kwa kutendeana mema ikiwa ni pamoja na kupata muda wa pamoja.

Pamoja na majukumu mengi ya kikazi, kazi isiwe sababu ya kudumu ya wanandoa kukosa muda wa pamoja.

Dhamira ya kutengeneza muda wa pamoja ikikosekana, muda hauwezi kupatikana. Kazi zisiondoe utu na thamani yetu katika familia.

Ni muhimu wakati wote kukumbuka kuwa kazi inatuhitaji, lakini familia inatuhitaji zaidi. Familia inahitaji sana uwapo wako.

Ukiona mwezi wako au watoto hawafurahii uwepo wako, ujue una matatizo. Wako wazazi ambao wanaweza kuwapo nyumbani lakini wasiwapo nyumbani.

Baba au mama kuwapo au kutokuwapo nyumbani haileti tofauti yoyote.

Familia haioni faida ya uwapo wa baba au mama. Tenda mema kwa familia yako ili siku zote uendelee kuishi katika mioyo yao na kubarikiwa.

Ndoa ni taasisi ambayo ni kitovu cha familia na malezi. Familia ndio msingi wa maadili mema kwani tabia na mienendo yetu inajengwa katika familia. Hata maadili ya viongozi yanajengwa kuanzia katika ngazi ya familia.

Pia maendeleo yanahitaji watu waadilifu. Uadilifu huo unajengwa katika familia kwanza. Kwa mantiki hiyo, ndoa zikiwa imara, kutakuwa na familia imara; kukiwa na familia imara kutakuwa na jamii imara na hatimaye taifa imara. Kwa maana hiyo, maendeleo ya taifa yanategemea ndoa imara.

• **Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi.**

**Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

MACHI 27, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana


*Jumapili*




Ukurasa 14

## MISHIKAKI YA KUCHOMA






Ukurasa 13

## MITINDO

GAUNI REFU

Linanoga kutembea mwendo wa paka




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# MNG'ARO WA HERENI

## Unaoambatana na uso wenye tabasamu

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M | K | A | T | E |
| | S | | | I | |
| K | O | O | | B | |
| | N | | V | U | A |
| | D | | | K | |
| K | O | M | B | A | |


## AMSHA AKILI



## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IGA, NMC, TAMKA, GAMBA, BINGWA, GOMBEA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

**Alichokifanya daktari**

MTOTO Juma alitaka kukwepa kwenda shule, alikwenda nyumbani kwa rafiki yake na kumuomba simu ampigie mwalimu wa darasa.

Bahati mbaya badala ya kumpigia simu mwalimu wake, aliweka namba ya mama yake.

Juma: Mwalimu tafadhali kesho sitakuja shule

Mama: We Juma kwa nini hutakwenda shuleni?

Juma: Mama anaumwa sana nataka kumpeleka hospitali, baba hajarudi nyumbani tangu juzi na hakuna mtu wa kumsaidia.

Mama: Mtoto acha uongo, mimi ni mama yako huo ugonjwa nimeutoa wapi?

Juma: Haa! Kumbe mama, nisamehe nitaenda shule.

**SWALI**

Pilipili inaongeza vitamini gani kwenye mwili wa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Huwezi kufanikiwa kwa kufanya kila kitu mwenyewe!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu kuhusu jinsi ya kuchagua marafiki zako. Tayari tumeona sifa za rafiki bora. Kwa wale ambao hawakubahatika kusoma mada zilizopita, nilitaja sifa kadhaa.

Sifa hizo ni pamoja na kuwa na rafiki mwenye hofu ya Mungu, rafiki anayekutia moyo wakati wote. Pia rafiki anayekudokeza siri ya mafanikio yake, rafiki anayekufaa wakati wa jua (wakati wa shida) na rafiki anayekutetea wakati wote.

Sasa baada ya kuchambua aina hizo za marafiki, leo tuangalie umuhimu wa marafiki au washirika. Mungu alipomuumba Adamu aliona si vyema aishi peke yake. " Bwana Mungu akasema, si vyema huyu mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."

Kiukweli, hakuna mwanadamu anayeweza kufanikiwa katika maisha kama atataka kufanya kila kitu mwenyewe. Hatukuumbwa kuishi na kufanya mambo peke yetu.

Maisha ni kutegemeana; ili kupata watoto, baba na mama watahusika. Ukiugua unahitaji daktari, mmoja anauza mwingine ananunua.

Tusipotegemeana, maisha yatatoweka. Fikiria dunia iwe ya wanaume tu au iwe ya wanawake tu. Ni dhahiri kwamba baada ya vizazi viwili wanadamu wangetoweka!

Hii inanikumbusha hadithi ya Robison Crusoe aliyeishi kisiwani peke yake kwa muda mrefu baada ya kuvunjikiwa na merikebu yake. Alikuwa akifanya kila kitu mwenyewe na hii ilimchukua muda mrefu kukamilisha jambo lolote.

Msomaji wangu, hebu sasa nikupe mifano michache ya watu waliofanikiwa katika maisha kwa kushirikiana na watu wengine.

Mtu wa kwanza ni Bill Gates, tajiri mkubwa kutoka Marekani alipoanzisha kampuni ya kompyuta ya Microsoft. Huyu alishirikiana na vijana wenzake tisa ambao hata ofisi hawakuwa nayo. Leo dunia nzima inatumia programu za Microsoft kwa ufanisi mkubwa.

Mtu wa pili tunayemfurahia ni Barack Obama kwa kuwa Rais wa kwanza mweusi nchini Marekani na kusifu uwezo wake wa kuhutubia. Tusisahau kwamba pamoja na uwezo mkubwa wa kuhutubia, alikuwa na timu mahiri ya watu waliomsaidia kufanikisha kampeni zake.

Hata hivyo, unapotaka marafiki au washirika wazuri ili kufanikisha malengo yako, zingatia mambo yafuatayo;-

Tafuta washirika waaminifu na watii. Unapotambua na kukubali kwamba huwezi kufanikiwa, ukifanya kitu mwenyewe ni muhimu kutafuta watu walio waaminifu, watii na wanaokubaliana na maono yako. Mzigo mzito unapobebwa na watu wengi, huwa mwepesi!

Pamoja na hayo, kupata watu waaminifu kunahitaji umakini, uangalifu na kumuomba Mungu akupatie watu hao. Watu wengi siyo waaminifu na usipokuwa makini watu hao uliowaweka karibu ndio watakaokugeuka na kukuangusha!

Jambo lingine la kuzingatia, tengeneza mfumo madhubuti mbali na mpango kazi niliotaja hapo juu ili watu ulioamua kushirikiana nao watimize majukumu yao. Ni muhimu kuwa na mfumo madhubuti wa utendaji ambao ukizingatiwa utaleta mafanikio.

Ni dhahiri kwamba timu inayocheza kwa kuzingati mfumo waliokubaliana, hutoka uwanjani na ushindi. Hata kama una wachezaji bora kabisa, msipokuwa na mfumo madhubuti wa uchezaji kushindwa ni dhahiri.

Hata hivyo, ukweli unabakia pale pale kwamba kuwapata watu watiifu na waaminifu ni hatua ya kwanza, na kuzingatia mfumo madhubuti wa utendaji ni hatua ya pili.

Uaminifu na utii vinapimika katika mfumo wa utendaji mliopanga. Mfumo huzaa mkakati utakaowezesha mafanikio kupatikana.

Wana wa Israel walipotaka kuupiga mji wa Yeriko, Mungu aliwapa mfumo na mkakati wa kushinda vita. Akili ya kibinadamu isingekubaliana na mfumo na mkakati huo.

Mpenzi msomaji wangu, tunapomshirikisha Mungu kwa kila jambo tulifanyalo, mafanikio ni dhahiri. Kwa matiki hiyo yatupasa kumuomba Mungu atupe mfumo madhubuti kwani hapo pana uhakika wa ushindi.

***Kwa leo niishie hapa. Wiki ijayo nijadili mambo zaidi ya kuzingatia katika kufanikisha malengo yako mazuri uliyo nayo iwe ni ya kibiashara na kadhalika. Kwa maoni, kisa cha kimaisha, tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# TARURA boresheni mfumo wa kukusanya maegesho

TANGU mwaka jana Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) ilikuja na utaratibu wa kutoza gharama za maegesho kwa mfumo wa kielektroniki ambao mteja anapata ankara yake kwenye namba yake ya simu.

Lengo ni kuwezesha mapato ya serikali yasipotee lakini madereva walipe kiwango halisi kinachotakiwa. Hii ni tofauti na awali ambapo ilikuwa rahisi kupotea na kuwaweka kwenye hatari wakusanyaji wa fedha hizo.

Utaratibu wa sasa ni mzuri kwa maana kwamba serikali inapata mapato kwa uhakika zaidi lakini unahitaji maboresho hasa kwa watenda kazi kwa kuwa wenye magari wanaumizwa.

Kiwango cha Sh. 500 kwa saa kinaweza kuonekana kidogo lakini wakati mwingine ni kikubwa kwa kuwa ikiwa kila siku unatozwa Sh. 2,500 kwa mwezi ni Sh. 75,000.

Kwa sasa unapoegesha gari anakuwapo mtu aliyevaa kikoti kilichoandikwa TARURA. Ananakili namba ya gari kwenye mfumo na kutoza fedha kwa kadri anavyoona na mwenye gari hapati ujumbe wala hawezi kuwa na uthibitisho wowote kuwa aliegesha gari eneo hilo.

Baadhi ya wakusanyaji hao wanachokifanya ni kumtoza mtu kwa kutwa ili wafikie lengo au unatozwa saa nyingi wakati hujakaa kwa muda huo. Wanasema wamejiongeza kuwa mwenye gari atakaa kwa siku nzima.

Wakati mwingine umeegesha gari kwa dakika tano ili uchukue kitu mahali, unamweleza kabisa kwamba unakaa chini ya dakika tano lakini anakutoza saa moja. Ukimuuliza kwa nini ametoza kiasi hicho, anasema hapana baadaye unakuja kupata ankara.

Hakuna anayebisha umuhimu wa kukusanya tozo ikiwa inakusanywa kihalali lakini kwa ilivyo sasa mwamuzi wa utozwe kiasi gani ni mkusanyaji kwa sababu anachoangalia ni kufikia lengo alilowekewa.

Bahati mbaya sana huwezi kupata ujumbe wa kwamba umetozwa kiasi gani, wapi na muda gani. Baada ya wiki au mwezi, ujumbe unaopokea ni kukumbushwa kulipa deni.

Ujumbe huo hutumwa kutoka 15200 ukisema: "Ndugu mteja, chombo namba..., deni la maegesho ni Sh... lipa kwa kutumia kumbukumbu namba,ili kuepuka kulipa faini."

Mteja huyu hana pa kulalamika anapotendewa ndivyo sivyo. Wakati mwingine hujaegesha eneo fulani unaletewa ankara ya maegesho na hii si sawa kabisa bali ni maumivu.

Kwa kuwa maeneo yenye maegesho hakuna kamera za kuthibitisha kuwa mhusika aliegesha gari eneo hilo, mwamuzi ni aliyewekwa na TARURA. Ni muhimu utaratibu wa kutoa stakabadhi na kuweka kwenye gari ukarejeshwa.

Mara kadhaa wakusanyaji hao wamedai hawatoi stakabadhi kwa sababu mfumo utamtumia mteja kwenye namba yake ya simu, jambo ambalo si kweli.

Kipindi cha nyuma ilikuwa kila baada ya saa moja, mteja anawekewa karatasi na analipa anapotaka kuondoka. Ni muhimu sasa karatasi zikawapo kuthibitisha deni husika kuliko kuondoka na hujui umeandikiwa kiasi gani.

Kama kuweka karatasi inaonekana haifai, basi ni muhimu mfumo ukaboreshwa ili mteja apate ujumbe ndani ya muda husika, namba ya gari yake inapoingizwa kwenye mfumo, lakini kuacha hivi ni kuumiza watu.

Pia yako maeneo mengine yanatozwa ambayo kimsingi ni ya huduma za kijamii. Mtu huenda kwa matatizo au ni muhimu lakini TARURA wanatoza tu bila kuangalia aina ya eneo husika.

Maeneo hayo ni hospitali na nyumba za ibada. Mathalani, wale wanaokwenda kazini asubuhi, mchana na jioni maana yake eneo lake la kazi kama mwajiri halipii maegesho anapaswa kulipa. Akienda ibadani kama napo hawana eneo la kutosha kuegesha nako anatakiwa kulipia.

Mmiliki wa gari binafsi ana tozo hizi na bado ana kodi mbalimbali kupitia kila lita ya mafuta anayoweka katika chombo cha usafiri. Kama ni dereva wa mtandaoni ana wajibu wa kulipa maegesho mara kwa mara anaposubiria wateja, analipa kibali cha jiji, manispaa, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na kodi ya mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).










Hivi ndivyo Mwenyekiti wa TLP, Augustine Mrema alivyowashtua Watanzania kwa kufunga ndoa na Doreen Kimbi katika kanisa Katoliki Parokia ya Uwomboni Kiraracha, mkoani Kilimanjaro.

# MITINDO





# GAUNI REFU LINANOGA KUTEMBEA MWENDO WA PAKA

KUTEMBEA ukiwa na gauni refu linalobana sio jambo rahisi, inahitaji kujifunza na kujiamini kuwa na mwendo mzuri.

Wanawake wengi wanashindwa kutembea vizuri wakiwa katika vazi hilo, mara nyingi wanajikuta wakipata aibu pale wanapokwenda kwenye sherehe au matembezi ya jioni yanayoambatana na burudani.

Kama ukihitaji kuwa na hali ya kujiamini na mtazamo wa kuvutia na gauni lako, jifunze jinsi ya kupiga hatua za paka maarufu kama 'CatWalk'wakati ukitembea.

Hizi ni baadhi ya dondoo unazotakiwa kuzifuata wakati umevaa gauni refu na linalobana mwili.

**JIFUNZE KUTEMBEA**

Usitembee kwa haraka au kujitingisha.

Chagua gauni ambalo litakufanya utembee kwa madaha, mwendo wa pole na wenye kukupa muonekano mtulivu. Hata kama gauni lako limetengenezwa kwa aina tofauti.

**VAA VIATU VINAVYOKUTOSHA.**

Kama unahitaji kuwa huru na raha zaidi katika miondoko ya kupendeza, unatakiwa kuvaa viatu vyenye visigino vya wastani. Ni vizuri kujiweka salama zaidi na muonekano mzuri kwa kutovaa viatu virefu kwani vitakufanya uwe mrefu na mwendo wa maringo kama Twiga.

Chagua kiatu kinachoendana na gauni na hakikisha gauni linaendana rangi na kiatu unachovaa kwani itakufanya kuongeza mvuto.

Jifunze kutembea mwendo wa paka

Unatakiwa kujifunza kwa ufasaha kutembea mwendo wa 'kukatika' ukipiga hatua kwa kuhesabu. Ni muhimu mtu maalum akawa anakuangalia jinsi unavyotembea ili kukufanya uwe na mwendo unaotakiwa.

**KUWA HURU NA JIACHIE**

Unatakiwa kutulia katika siku yako hiyo muhimu, ukifanikiwa hilo kila kitu kwako kitakuwa rahisi. Usihofu kuhusu kutembea muda wote, au jinsi ya kusimama bali fanya jambo hilo kama rahisi.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# MNG'ARO WA HERENI

## Unaoambatana na uso wenye tabasamu





HERENI ni pambo linalovaliwa masikioni na kwa kiasi kikubwa linachangia kuongeza mvuto na muonekano mzuri wa sura.

Kuna aina nyingi za hereni katika tamaduni mbalimbali.

Zipo ambazo hutengenezwa kwa kutumia vito vya thamani kama vile dhahabu, almasi, rubi au shaba.

Vilevile zipo ambazo hutengenezwa kwa kutumia malighafi za asili kama vile mbao, vifuu vya nazi, mfupa, kioo na shanga.

Hereni zilizotengenezwa kwa shanga zimekuwa zikiwavutia watu wengi kuvaa kutokana na nakshi zake za asili.

Mara nyingi uvaaji wa hereni unatakiwa kuzingatia aina ya nguo uliyovaa, hapo unatakiwa kucheza na rangi.

Mpangilio wako wa nguo na hereni utakufanya uonekane maridadi na sura ang'avu yenye tabasamu pana.

Unapotoka kwenda katika shughuli zako au uwapo nyumbani basi zingatia uvaaji wa hereni.

Uvaaji usiozingatia mpangilio wa rangi na hereni zako huondoa ladha ya urembo na si rahisi kwa mtu mwingine kugundua umependeza.

**ANGALIZO**

Epuka kuvaa hereni zaidi ya moja katika tundu la sikio kwani kufanya hivyo kunaweza kupelekea ukubwa wa tundu kuongezeka na hatimaye nyama ya sikio kuchanika.

Hereni nzito sana nazo huchangia kutokea kwa tatizo hili.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# MISHIKAKI YA KUCHOMA

MISHIKAKI ya kuchoma inakuliwaza na kukupa raha ya maisha.

Ni rahisi kuandaa, inafaa kuliwa vizuri taratibu ukiwa umepumzika nyumbani wakati unapata kinywaji cha kukupa afya na familia.

Mahitaji

Nyama kilo mbili, ikiwa kwenye vipande vidogo vidogo, nyanya moja, menya na kata vipande, tangawizi moja kata vipande vidogo, kijiko kimoja cha cumin ya kusaga, karafuu nne, limao moja na mafuta ya kula kijiko kimoja.

Coriander nusu kikombe, pilipili mbuzi mbili, kijiko kimoja cha paprika, bizari nusu kijiko na chumvi.

Namna ya kuandaa

Changanya kila kitu, kasoro nyama, kwenye blender na kisha saga vizuri.

Chovya nyama vizuri ili ipate kulowa vizuri na weka nyama iliyochovywa kwenye jokofu usiku mzima ili kupata matokeo mazuri zaidi.

Choma nyama kwenye jiko la mkaa ili kupata ladha halisi, ni vizuri kama utaweka pilipili hoho na karoti ili kuipa mishkaki muonekano mzuri na kuongeza utamu.

Unaweza kula na mkate au kitafunwa chochote kinachokufurahisha.



# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Kuwa mbunifu kupangilia vitu kwenye nyumba ya eneo dogo

## Namna ya kuchagua sofa ya sebule



Namna ya kuchagua sofa ya sebule
KATIKA sebule inapendeza kama kutakuwa na viti aina ya sofa kwa ajili ya kupumzika au kukaa wageni wanaowasili kila mara. Kwa kawaida wakati unataka kununua sofa lazima uzingatie vitu vingi ili kupata bora na inayodumu kwa muda mrefu.
Kutokana na umuhimu wake, zifuatazo ni baadhi ya dondoo ambazo zitakuongoza kupata sofa inayokubalika.

1: Hakikisha unaangalia muundo wa sofa kama unakidhi na kupendezesha sebule yako. Hii ni kuangalia ukubwa na ubunifu wake.
2: Chagua sofa yenye kitambaa au ngozi halisi katika kukupa uhakika wa kudumu kwa muda mrefu.
3: Rangi ya sofa ni jambo muhimu la kuangalia kabla ya kununua. Tafuta ushauri kwa watu wenye taaluma ya upambaji ili akusaide rangi inayoendana na ukuta wa sebule.
4: Angalia unafuu wa bei kama unaweza kuimudu, kama pesa zako ni pungufu ni bora kwenda kuongeza kidogo kidogo ili kupata sofa nzuri na imara.

ASILIMIA kubwa ya wakazi wanaoishi mijini wanaishi katika nyumba za kupanga.

Kutokana na hali halisi ya familia za kiafrika, ni chache sana ambazo huwa na uwezo wa kumudu kupanga nyumba yote au kubwa ya kutosheleza familia nzima.

Kama ilivyo desturi kwa familia hizo za kiafrika, nyingi huwa zinajumuisha zile kama zinazojulikana kwa lugha ya kigeni 'extended family' na hivyo familia kuwa kubwa pasipo kulingana na kipato kilichopo cha kumudu kupanga nyumba kubwa.

Kwa hiyo ili umudu kuishi katika sehemu ndogo ya nyumba kulingana na uwezo uliopo na ukubwa wa familia iliyopo lazima ubunifu na akili nyingi utumike katika kupangilia vitu ili nafasi katika nyumba hiyo itosheleze mahitaji.

Pia kuna haja ya kupunguza kuweka ndani ya nyumba baadhi ya vitu visivyo vya lazima.

Kwa upande wa uwekaji wa samani katika nyumba hiyo ndogo, ni lazima uhakikishe kwamba zenye umbo dogo na ambazo zitakuwa na sehemu ya kuhifadhia vitu vingine au zenye matumizi zaidi ya moja.

Kwa mfano meza ya televisheni, unaweza kuweka ambayo inakuwa na matumizi ya kuwekea TV na pia kwa kuhifadhia vitu vingine hususani vitabu.

Pia kutumia sehemu ya ukuta 'kudizaini' kwa ajili ya kuwekea vitu vingine ikiwamo vyombo hasa jikoni.

Na ili ufanikishe kwa vitu vichache unavyokuwa umepanga kuweka kwenye nyumba hiyo ndogo, ni vizuri kupima kwanza ukubwa wa eneo lako kabla ya kutengeneza samani zako.

Epuka kuweka vitu hovyo bila kufanya tathmini ya uhakika na ikiwezekana orodhesha idadi ya vitu na vya aina gani vinavyotakiwa kuingia kwenye nyumba hiyo na ambavyo havichukui nafasi kubwa.

Tumia ubunifu katika sehemu za kona za nyumba yako kuweka fanicha zako, hususani meza na televisheni na uhakikishe nazo zinakuwa ni zile ambazo hazichukui nafasi kubwa.

Jambo kubwa la kuzingatia katika suala la kupangilia vitu katika nyumba yako ndogo ni ubunifu na kuepuka vitu ambavyo havina ulazima.


Usiweke kitu ili mradi umeona kwa jirani yako ameweka isipokuwa kwa kuzingia umuhimu wake na nafasi uliyo nayo kwenye nyumba yako.

Pia katika siku za hivi karibuni kwa upande wa samani za ndani, ziko hata ambazo unaweza kuzikunja na ukifanikiwa kupata za namna hiyo, inakuwa bora zaidi katika kuhifadhi nafasi.

Kwamba unazitumia pale unapoona inahitajika tu na unaweza kuamua kuzikunjua nyakati za mchana halafu usiku ukakunja.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MUME WANGU, SHOGA'ANGU KAJUAJE KAMA NAMUHISI KUWA UNATEMBEA NAE WAKATI SIJAMWAMBIA MTU ZAIDI YAKO?
ULINIULIZA KAMA 'FRIJI LANGU LINA-GANDISHA?'
!?
WAPIGA DILI
'TULIA HUKU!' ACHA KIHEREHERE!
USIONDOE GARI ANAJIFANYA MWENDAWAZIM ATOAGI NAULI
NIKUO-NESHE KITAMBU-LISHO?
KITAMBULISHO CHA CHIZI NI MATENDO YAKE WE'HANGAIKA TUUMIZWE!
STENDI YA BASI
WEWE RUHUSU GARI BHANA UNATULAZA!
NA WEWE MWANDAAZIM TULIA!
NITALIWEKA WAPI BANDA LA BATA, JIKO LANGU LA KUNI?
HA HA HAAAA HE HEE!
TUSHIKIENI HA HAAA!
MIGOMIGO
NTAMISI KUSUTANA!
TUWAHI KABLA HAWAJAWAHI
NA WEWE ULIFUATA NINI MPAKA UMUONE MKE WANGU GESTI?
UNEPENDEDHA!
UDHURI UNACHANGIA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...USINENE UKAMALA

## RIPOTI YA KAMATI

# Wataalamu watoa ufafanuzi zaidi

INATOKA UK. 2

matetemeko yaliyowahi kutokea kama inawezekana kuna miamba imepasuka mafuta yakatoka kutoka chini lakini taarifa zinaonyesha hakuna matetemeko makubwa yaliyowahi kutokea kusababisha kupasuka kwa ardhi,"alisema.

Vilevile, alisema taarifa za miamba zilipitiwa na kujiridhisha kwamba miamba ni ya zamani na haionekani kulalia uozo wowote wa viumbe hai.

"Haiwezekani kukawa na petroli, kinachofuata sasa ni kuchukua sampuli kupeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali 'hebu tupimie kiundani tujue mafuta haya chanzo chake ni nini?' Taarifa zikaja zikaeleza kwamba hayo mafuta hayana viini vya petroli, kiini kikubwa ni mafuta yatokanayo na mimea," alisema.

Alibainisha kuwa Maabara za Mkemia Mkuu wa Serikali Dar es Salaam na Mwanza, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) na Mamlaka ya Maji Bonde la Ziwa Victoria walitumika kupima sampuli hizo za mafuta.

"Taasisi zilizoandikiwa barua na kamati ni pamoja na GST, TPDC tuliwaandikia watuambie kama kuna uwezekano wa mafuta Mto Mara walisema hakuna.

"Tulimwandikia RMO (Mganga Mkuu wa Mkoa) 'hebu tueleze kama kuna taarifa za magonjwa yatokanayo na kuchafuka kwa maji kuanzia Februari Mosi mwaka huu kabla mvua haijanyesha hadi tarehe 13/3/2022 tulipoanza kazi ya utafiti', tulipewa taarifa tukachakata hakukuwa na mlipuko wowote.

"Tulimwandikia mwenzetu wa Bonde la Maji Victoria 'tupe taarifa za mvua kwa miaka mitano iliyopita', flow ya maji mtoni, taarifa za kimaabara walizofanya kabla ya kamati kuanza kazi zikaletwa, tumechakata," alisema.

### VIJIJI VILIVYOHUSISHWA

Alisema vijiji vilivyohusishwa kuwapa taarifa kwa kutumia dodoso na majadiliano na wanakamati ni Kirumi, Ryamisangana, Kitakaswa, Wegero (Wilaya ya Butiama), Kwibuse, Kwibwe, Bisarwi, Kuruya (Wilaya ya Rorya) na Nyabichume, Matongo, Mjini Kati (Nyamongo) na Mrito (Wilaya ya Tarime) na kuongea na wananchi.

"Hizi wilaya ndio zinazopakana na eneo oevu, kulikuwa na madodoso ya jumla 90, wafugaji 15, wavuvi 23, wakulima 30, wengine 19, madodoso 177 yalijazwa," alisema.

Alibainisha kuwa waliitisha taarifa idadi ya mifugo kwa kata zilizokaribu na Mto Mara ambapo inaonyesha kulikuwa na ng'ombe 300,002, mbuzi 88, 000 na kondoo 72,000.

"Sasa ni nani walioingia kule? Hatusemi kwamba ni wenyeji peke yao, mifugo ilitoka hadi mikoa mingine kuingia kwenye eneo lakini chanzo kikuu ni tope chini ya maji," alisema.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya kuchunguza chanzo cha kuchafuka kwa Mto Mara, Prof. Samweli Manyele, akieleza sababu za kuchafuka kwa mto huo, jijini Dodoma jana, baada ya kukamilika kwa taarifa ya kamati hiyo, iliyoundwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo Machi 12, 2022. Kushoto ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga na Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), Edward Nyamanga. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

### MATOKEO YA UCHUNGUZI

Mwenyekiti huyo alisema walishuhudia uwapo wa utando wa mafuta juu ya maji ambapo vipimo mbalimbali vya awali vya ubora wa maji vilionyesha uwepo wa kiwango kikubwa cha mafuta na vilainishi (oil & grease) ambavyo viliwalazimu kufanya utafiti wa kina kujua aina ya mafuta yaliyokuwapo kwenye maji ya Mto Mara.

"Tulisema kama ni hivyo hizi sampuli zilizoonyesha mafuta, tufanye uchunguzi wa kina na tulipata matokeo yanayoonyesha kwamba mafuta yale yanatokana na kuoza kwa mimea na sio petroli.

"Kawaida maji yanatakiwa kuwa na oksjeni kuanzia kiasi cha miligramu nne hadi nane, samaki wanaishi na viumbe vinaendelea kuishi. Tulichokiona sehemu nyingine kwenye maji, oksjeni ilikuwa inasoma sifuri, maana yake ni kwamba hapo samaki hawawezi kusalimika.

"Hii ndio sababu kubwa iliyosababisha vifo vya samaki, kwa sababu tulipoangalia taarifa za minofu ya samaki matumbo ya samaki hakukuwa na sumu yoyote sababu iliyobakia ni hii ya kukosa hewa ya oksijeni," alisema.

Alitaja visababishi vya kukosekana kwa oksjeni kuwa ni mmeng'enyo wa viumbe mfu chini ya maji ambavyo ni mimea iliyooza na imekaa kwa muda mrefu.

"Kitu kingine, kinyesi kikiingia kwenye maji, kwenye kumeng'enywa kinatumia oksjeni, kinatengeneza mishefeni ambayo inatengeneza kabonidaioksaidi," alisema.

Alibainisha kuwa rangi nyeusi pia inachangia kuzuia mwanga kuingia kwenye maji, hivyo mimea inayotumia mwanga kuishi inakosa nafasi ya kuishi, kuna athari kwenye mfumo wa utengenezaji wa chakula kutokana na tope kutibuliwa na mvua kubwa iliyonyesha.

Kuhusu usalama wa visima vilivyo kando ya Mto Mara, alisema walichukua sampuli kwenye visima na kuonyesha kutokuwapo kwa madini yenye madhara ya afya kwa binadamu kulinganishwa na viwango vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Afya Duniani (WHO).

"Tulishauri uongozi wa Mkoa wa Mara kuwatangazia wananchi na waziri alikuja Musoma na kumweleza Mkuu wa Mkoa ili kuwatangazia wananchi, 'maji ya visima endeleni kutumia'," alisema.

"Kinachotokea ni kwamba mto unaweza kujisafisha wenyewe endapo mvua itaendelea na tabia ya mito kuchafuka wakati wa mvua inajulikana duniani, ikinyesha mvua halafu ikaendelea mto unajisafisha wenyewe.

"Tulipowauliza wananchi, walisema huwa inajitokeza tabia hiyo lakini mwaka huu imekuwa kubwa zaidi. Ni kwa nini? Sababu ni kwamba mwaka 2021 ilitokea mvua kubwa na tope likazagaa lakini kwa kuwa mvua iliendelea tope lilipotea na mwaka huu kilichotokea ilinyesha mvua kubwa na haikuendelea tena hadi tunavyoongea hivi.

"Mto umebaki unasubiri mvua kuweza kujisafisha wenyewe, hili ni tatizo ambalo tunaomba tueleze na hiki ndicho chanzo kikubwa cha kuchafuka kwa Mto Mara, maji hayakuongezeka ili kubeba taka, ndiyo maana taka zimebakia pale," alisema.

Alibainisha kuwa eneo ambalo uchafu unaanzia wameangalia kina cha tope, kuna mita 100 kutoka kwenye usawa wa maji hadi chini ya mto.

"Kina kile ni kirefu, tope ni jingi. Kwa hiyo lilipotibuliwa, hili linatofautiana maeneo mengine, ndiyo maana tope limekuwa jingi likasambaa kwenye maji," alisema.

### KWINGINEKO DUNIANI

Alisema kamati iliangalia maandiko mbalimbali ya kuchafuka kwa mito duniani ambapo ilionyesha hata Congo, Rwanda, India, Cameroon, Bangadesh na Australia wamewahi kukumbwa na hali kama iliyotokea nchini na samaki wakafa.

Alisema sababu za kuchafuka kwa Mto Mara ni tope kuwa jingi kuliko kinyesi na kudai kuwa kinyesi kinaongeza mbolea na kuyafanya magugu maji yazidi kukua na kuongezeka.

"Taarifa tuliyowaletea ni kwamba Mto Mara haukuchafuka kwa kemikali, bali kwa tope," Prof. Manyele alifafanua.

### MAPENDEKEZO SERIKALINI

Mwenyekiti huyo alisema shughuli za jamii ambazo ni rafiki kwa mazingira zilizokuwa zinafanyika kwenye ardhi oevu ya mto ziendelee kama iliyokuwa awali.

Alisema rangi nyeusi kwenye maji inatarajiwa kuendelea kuwapo kwa muda hadi mvua zitakaponyesha na kusafisha mto, hivyo maji yanafaa kutumika kama yatatibiwa.

"Tumeshauri kuwe na mchakato wa ardhi oevu ya Mto Mara kutangazwa kama eneo la hifadhi kutokana na upekee wake. Tumeangalia sheria zinazoweza kutumika, mchakato wake haukuwa sehemu ya kazi yetu, tumeshauri baadaye kama inawezekana mchakato ufanyike, kuna mambo ya kuangaliwa kwenye hili eneo, mifugo ipewe nafasi yake lakini pia litengwe na kuhifadhiwa," alisema.

Pia alisema utafiti mwingine wa Bonde la Mto Mara uendelee kwa kuwa wamebaini uelewa wa Watanzania juu ya sayansi ya Mto Mara ni mdogo.

"Hii kazi iliyofanyika iamshe sasa utafiti mwingine na tukataja vyuo vinavyoweza kuingia kwenye utafiti wa aina hiyo, wananchi walipo karibu na mto wapewe vyanzo mbadala vya maji kama visima na maji ya bomba, ili kupunguza utegemezi wa maji ya mto, walio kuwa wanatumia mto walipoambiwa hawawezi kutumia tena ilisababisha taharuki,"alisema.

Alishauri serikali itengeneze mpango wa kujenga visima kwa kuwa wananchi wengi wanatumia maji ya mto huku visima vikiwa vichache kwenye eneo hilo.

"Wakati tunachukua sampuli za visima, tulitembea kwa gari umbali wa dakika 50 ndiyo ukute kisima kingine kwa sababu wao wanatumia mto, visima ni vichache sasa, ikitokea taharuki itakuwaje? Tukashauri visima viongezwe," alisema

Pamoja na hayo, alisema kuna umuhimu wa kuanzisha programu ya pamoja ya uhifadhi wa ardhi oevu ikihusisha sekta za mazingira, ardhi, maji, maliasili, mifugo na uvuvi.

Alisema wameshauri namna ya kupambana na magugu maji kitaifa ikiwamo kuyavuna kwa kuondoa kwenye mto au kutumia wadudu rafiki waliokuzwa kitaalamu kuyala magugu hayo.

### UFAFANUZI ZAIDI

Mjumbe wa kamati hiyo kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Daniel Ndio, alisema mafuta ya mimea yaliyobainika ni kidogo.

"Uchunguzi wa kina umebaini mafuta hayo ni ya mimea na ni kidogo sana ambayo yapo chini ya kiwango cha kitaifa, pia kuhusu uozo wa majibu ya Maabara ya Mkemia Mkuu, tuna kemikali iliyobainika kwenye vipimo vya sulphur ipo juu sana hadi kiwango kinachofika 2,000 hadi 5,000 wakati kiwango cha kitaifa inatakiwa kuwa 500," alisema.

Alibainisha kuwa kiwango cha sulphur kinatokana na gesi ambayo inatokana na uozo na kukiwa na uozo wa aina hiyo, kunasababisha harufu inayofanana na yai lililooza.

"Samaki walikosa oksjeni kutokana na kuwapo na shughuli nyingi za wadudu ambao walikuwa wanatumia ile oksjeni katika kumeng'enya ule uchafu na matokeo yake oksjeni ikawa haipo na ndiyo maana maeneo mengine inasoma sifuri kwa kuwa ilikuwa inatumika kumeng'enya uchafu,"alisema.

Akizungumzia hali halisi ya uozo unaotokea chini ya maji, Mtaalamu kutoka Idara ya Kemia ya UDSM, Dk. Kessy Kilulya, alisema kwenye mto kuna magugu mengi yanayoishi na kufa.

"Mvua inapokuja kwa kile kilichotokea ni kwamba yale magugu yaliyokufa, yalisukumwa kwa wakati mmoja hadi kuingia kwenye maji, wadudu wakaanza kuyashambulia.

"Sasa ile 'decomposition matter' (kitu kilichooza), bakteria wanatumia oksjeni, inachukuliwa kwa wakati mmoja kwa kasi kubwa na wenyewe wanaongezeka zaidi na ndipo oksjeni ikashuka na tukaona ikawa sifuri," alisema.

"Uwapo wa madini tembo hasa aina ya chuma, unaungana na ile 'minimum possible unique substance', inatengeneza 'complex compound' ambazo kwa kawaida zinatoa rangi na hii ndio chanzo cha rangi kwenye mto, na hii inatokea kwenye mito yenye 'high organic matter'," alisema.

Katika kikao hicho, wajumbe wa kamati hiyo waliambatana na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga.

## MAKALA

# SI KILA ANAYEKUSIFU NA KUKUPONGEZA NI MWEMA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

KUSIFU na kupongeza kunaweza kuwa njia mojawapo inayoweza kutumika kama kipimo kwa yale unayoyafanya. Ukisifiwa juu ya jambo fulani ulilofanya, inaweza kukupa ari ya kufanya zaidi.

Ukipongezwa vilevile kunaweza kuongeza ari ya kufanya zaidi. Jambo moja muhimu ni kuwa na uhakika juu ya yale unayosifiwa na kupongezwa kama unastahili au la.

Nakumbuka kisa kimoja wakati bado naishi nyumbani kwetu. Siku moja mdogo wangu wa mwisho kuzaliwa alitoka shuleni, wakati huo akiwa darasa la nne. Haikujulikana kama alinunua au alipewa ndizi njiani lakini alikuja nayo mpaka nyumbani. Alipofika tu akamkimbilia baba yetu akampatia ile ndizi.

Kilichotushangaza ni kwamba badala ya baba kufurahi kwamba mtoto kaonyesha upendo, alimwagiza akalete fimbo.

Alipoleta, mzee alimwambia lala chini, akamtandika viboko kama vitatu akamwambia simama.

Baada ya hapo alimwamuru amwambie kwa nini anampatia ndizi. Katika hali ya kawaida tukashangaa sana, tukawa tunajiuliza huyu mzee vipi je, hampendi mwanaye au tatizo nini? Kilichotokea ni kwamba bwana mdogo yule alieleza kwamba amepoteza mtihani wake wa Hisabati na Kingereza.

Kumbe hakuwa amefanya vizuri katika masomo hayo na hakutaka mzee afahamu.

Akaona amzubaishe na upendo wa ndizi kama rushwa ya kumfumba. Lakini mzee kwa sababu alikuwa na saikolojia ya hali ya juu, akawa ameshagundua mchezo nasi tukasema ahaa kumbe ndiyo maana na tukaondoa shaka yetu dhidi ya mzee.

Ndivyo ilivyo pia katika maisha ya kawaida ya binadamu. Tutakubaliana kwamba kila binadamu amezaliwa na roho ya ubinafsi, kinachotokea ni kwamba tunazidiana kiwango.

Ukitaka kujua, tazama maisha ya watoto wadogo. Mtoto mdogo kila anachokiona anataka kiwe chake au apate zaidi ya mwingine.

Ukitaka kufahamu zaidi ni wakati wa kula. Kuna baadhi ya watoto kula peke yao huwa hawataki.

Wanasumbua sana. Sasa ukiona anasumbua, ita watoto wa jirani waweke pamoja uone kama hawajaagiza ugali mwingine. Ukishawaweka pamoja, tenganisha sahani zao, utaona kila mmoja kabla hajaanza kula anachungulia kwanza kwenye sahani ya mwenzake kutaka kupata uhakika kama hajapunjwa.

Atakayegundua kwamba amewekewa kidogo, utaona anaanza kubadilika na kujigalagaza na mwisho atakataa kula.

Kwa sababu ya ubinafsi huu tulio nao, huwa ni ngumu na mara chache wale wanaokusifu na kukupongeza, hufanya hivyo wakiwa wanamaanisha.

Wako wanaokupongeza na kukusifu hadharani kwa sababu kuna mambo wanataka kuyaficha.

Wako pia wanaofanya hivyo kutaka kupata vitu kutoka kwako. Wako watakaokusifu hadharani lakini pembeni wanakusema vibaya na wengine wanafanya hivyo wakijua kwamba unakosea ili ukosee zaidi baadaye wakucheke.

Sina maana kwamba tusiwasifu watu au kuwapongeza pale watakapokuwa wamefanya vizuri lakini kwanza pongezi hizo lazima ziwe na maana halisi na si vinginevyo.

Lakini pia unayepongezwa ni muhimu kutafuta kwa nini unasifiwa na kupongezwa sana. Usipogundua unaweza kuvimba kichwa kwa kudhani uko sawa.

Jambo hili la kusifu na kupongeza kwa miaka ya hivi karibuni, limeonekana sana katika eneo la siasa na uongozi wetu. Wale wanaopiga zumari za kusifu na kupongeza kila wakati viongozi wa juu, baadhi yao tumeshuhudia wakiteuliwa kwenye nafasi mbalimbali.

Wengine walikwenda mbali zaidi kiasi cha kutafsiriwa kama walifanya kufuru katika kuwasifu baadhi ya watu na kuonekana kama wako kwenye nafasi ya uumbaji.

Kuna wakati sifa na pongezi zikizidi, huwa zinapofusha yale tunayofanya huku tukidhani tunayapatia.

Mwaka 1994, nikiwa shule ya msingi, baba yangu alininunulia viatu vikiitwa Maradona vya rangi ya njano na mistari mieusi, meno chini kama hizi njumu za siku hizi.

Nilipokwenda nacho shuleni, karibu wanafunzi wote shule nzima kuanzia la kwanza mpaka la saba, hakuna aliyekuwa anavaa viatu isipokuwa sisi watoto wachache.

Kwa hiyo wenzangu wakaanza kunisifu "kiatu kizuri sana ebu piga hiki kisiki kama utaking'oa". Nami mwamba staki kuonekana nitashindwa, basi nikaonyesha uimara wa Maradona, nikapiga kisiki nikavunja dole gumba la mguu, ikabidi nijikaze kisabuni wasije kunicheka nikaenda kuugulia maumivu nyumbani.

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba sifa na pongezi zimewapoteza watu wengi katika kazi zao. Kwenye nafasi za madaraka ndiyo kabisa. Mtu akisifiwa anataka wamjue yeye ni nani.

Anataka ajulikane yeye si wa mchezo mchezo na kwamba ni mwamba.

Lakini jamaa wakikaa gizani wanamcheka chini chini na kama huna saikolojia ya kuwafahamu watu, utajikuta wakati mwingine ukionekana mjinga kwa kuaminishwa kwamba wewe ni jembe.

Ukisifiwa na kupongezwa, shukuru, songa mbele kwa umakini mkubwa.

Ukiwa kiongozi, sifa na pongezi zisikufanye usiwe mkweli kwa wale wanaokusifia pale wanapokosea.

Ni bora ukawa na watu wachache kwenye taasisi wanaokusifu na kukupongeza na uwe na watu wengi wanaothubutu kukwambia ukweli juu ya makosa yako kiutendaji kama kiongozi.

Ninasema hivyo kwa sababu mambo yakishaharibika, wale wale waliokuwa wakikusifu wanaungana na wale waliokuwa wanakukosoa na kukwambia ukweli. Tena utasikia wanasema sisi tulijua hatoboi. Sasa mbona hamkumwambia? Huo ni unafiki.

Wakosoaji hukuimarisha zaidi kuliko marafiki wanafiki. Waandishi wa habari na vitabu wataneilewa zaidi kwa sababu tunajua tulikotoka katika kazi ya uandishi tumekosolewa sana juu ya lugha, mpangilio wakati mwingine hata hoja zenyewe na bado tunaendelea kujifunza.

Kwa hiyo siyo kila anayekusifu na kukupongeza ana nia njema. Pia si kila anayekukosoa na kukushauri ana nia mbaya. Wengine wanakutakia mema, hivyo muhimu ni kuwa na tafakuri ya ndani zaidi kuujua ukweli wa kwa nini unasifiwa na kupongezwa.

**0689157789**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mbaraka alipoamua kujiimba mwenyewe



Na Adam Fungamwango

MARA nyingi wanamuziki wa zamani walikuwa wakitunga nyimbo kwanza kabisa hisia tu, pili kwa kuangalia matukio na matendo yanayojitokeza kwenye jamii.

Lakini kwa asilimia 80, nyimbo zao nyingi zilikuwa za matukio ya kweli kabisa. Kama hayakuwatokea wao, basi yatakuwa yamewatokea rafiki zao, ndugu zao, wapenzi wao au watu wao wa karibu.

Ndiyo maana nyimbo zao huwa hazichuji na zinaendelea kuishi. Nasema zinaendelea kuishi kwa sababu kama wimbo ulitungwa kwa ajili ya tukio lililomtokea kweli mtu fulani, basi litaendelea kumtokea mwingine siku nyingine, mwaka mwingine na litajirudia miaka na miaka kwa wengine.

fano Maximillian Bushoke alimtungia wimbo rafiki yake Bokasa aliyefiwa na mkewe Aminani Mandari waliokuwa wakiishi mtaa wa Mafere maeneo ya Kinondoni Garden, Dar es Salaam katikati ya miaka ya 1980, ukaimbwa na bendi ya Orchestra Safari Sound 'Ndekule'. Wimbo kama huo ukiimbwa hata sasa na akausikia mtu ambaye amefiwa na mkewe, ni lazima atapata simanzi tu.

Maisha ya binadamu ni yale yale na yanajirudia. Linalompata huyu, ujue kesho litampata mwingine ndiyo maana nyimbo za zamani huwa hazichuji.

Nyimbo zinazochuja ni zile ambazo msanii au mwanamuziki anaamua kujitungia tu, hazimgusi mtu wala jamii. Huo hauendi mbali. Tunaziona baadhi ya nyimbo hasa za kisasa, zinatamba kwa wiki mbili tu, baada ya hapo huzisikii tena.

Leo nitauzungumzia wimbo mmoja ambao Mbaraka Mwinshehe Mwaruka aliamua kujiimba mwenyewe. Baada ya kuimba mikasa aliyoiona au kupewa na rafiki, ndugu na jamaa zake, huu sasa aliyeutunga mwanzoni mwa miaka ya 1970, akajiimba na kujikosoa. Unaitwa 'Kigeugeu'.

Duru za muziki na baadhi ya watu wa karibu yake, wanasema kuwa Mbaraka ambaye asili yake ni Mzenga mkoani Pwani ambako ndiko alikozikwa, alitoka Morogoro na kwenda kwao kusalimia wazee na ndugu zake. Alipofika katika pitapita yake, akakutana na msichana mmoja mrembo, akavutiwa naye.

Hata hivyo, msichana huyo hakupinga wala kukataa. Akamwambia kwa sasa hawezi kukubali lolote na kama anampenda kweli basi aende kwa wazazi wake akajitambulishe. Akifanya hivyo tu, basi hatakuwa na kipingamizi kwa sababu hata likitokea la kutokea, labda ujauzito, basi watajua ni wa nani.

Hiyo kwake Mbaraka ikawa ngumu kidogo lakini akamsisitizia kuwa yeye hana nia mbaya kwani lengo lake ni kumuoa baadaye. Msichana akashikilia msimamo wake na kumwambia tatizo la wanaume wengi ni wadanganyifu, ahadi zao za uongo, hivyo anaogopa kufanya chochote kwa sababu anaweza kurudi Morogoro akapata mwanamke mwingine na kumsahau. Mambo yakashindikana.

Mbaraka baada ya likizo akarejea Morogoro. Mwaka uliofuata alikwenda tena kwao Mzenga lakini safari hii akiwa na mke. Huyo ni Amney Shadad au Amney Mbaraka ambaye alifariki dunia mwaka jana. Wakati yuko kwenye matembezi, alishtukia akiitwa na mtoto, akamwambia anaitwa na mwanamke mmoja. Alipokwenda kumwangalia alishtuka. Ni yule yule wa mwaka jana.

Akamuuliza kiko wapi? "Habari zako ninazo, umeona?. Si nilikwambia? Si Ungenileteа tu matatizo?" Kisa hicho Mbaraka hakukiacha hivyo hivyo. Akaamua ajiimbe kwa tukio alilolifanya. Ndipo ulipotokea wimbo wa 'Kigeugeu' ambao mashairi yake ni haya hapa.

"Naogopa utanipoteza, utaisumbua roho yangu. Naepuka kigeugeu, nyinyi wanaume ahadi hamna. Naota nitakuja kujuta, utakuja kupata mwingine na kunisahau.

Twende sasa kwa wazazi wangu, wakutambue ewe bwana, kama wanipenda. Bila hivyo we bwana sina haja nawe, ndoa haipendi kufanya hivyo, uhuni sitaki."

Mbaraka alifariki dunia Januari 12, 1979 nchini Kenya lakini wimbo wake huo bado unaishi. Kwa sababu watu wenye tabia hiyo wako wengi tu na wataendelea kuwapo, kikubwa ni kwa kinadada kuwa makini na misimamo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-23

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

MPIGAJI alikuwa mahiri kwani hata sura ya dereva ilionekana vizuri tu pamoja na namba zake za usajili, Eddy alikuja kuliona kwa macho yake kwenye Pub ya Fabrice huko Tegeta, siku aliyoahidiana kukutana na Mwahija.

Alipoliona alilifananisha na gari ambalo liko kwenye picha aliyopewa na Nanje. Na kweli alipoangalia hata namba zake zilifanana na lile gari lenye rangi nyeupe aina ya Toyota Alphard ambalo picha ilitumwa kwake.

Itakumbukwa aliingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake ya mkononi. Akatafuta picha moja akaiangalia.

Ilikuwa picha ya gari lile na namba zilikuwa zile zile. Alisaka picha nyingine aliyokuwa na wasiwasi nayo. Nayo ilikuwa picha ya gari lile lile.

Aliteremka dereva kijana ambaye alionekana na umri kati ya miaka 26 na 30 hivi. Alivaa suruali aina ya 'Jeans' na fulana ya rangi ya bluu.

Alishuka ndani ya gari hilo peke yake. Bila hili wala lile, aliingia kwenye pub hiyo.

Akalipiga picha gari hilo, akawa na picha tatu za gari lile lile zilizopigwa sehemu tatu tofauti.

Ndilo lililopigwa picha na Nanje na yeye mwenyewe aliwahi kulipiga picha kabla.

Ni siku ya kwanza kwenda Tegeta na kuonana kwa mara ya kwanza na Mwahija.


Baada ya mazungumzo alimwomba ampeleke nyumbani kwa Chilambo akaangalie nyumba aliyodai 'mpwa' wake Tina anafanyia kazi.

Alipokuwa akishangaa uzuri wa nyumba hiyo, ndipo Eddy alipopiga picha mandhari ya ndani ambapo magari mawili yalikuwa yamepaki.

"Hii ndiyo nyumba ya marehemu Hafidh Chilambo." Mwahija alimwonyesha Eddy jumba moja la fahari lililokuwa na geti jeusi.

Pembeni kulikuwa na kikaratasi chenye maandishi kuwa wanauza barafu, maji baridi na 'ice cream'.

"Okay, kumbe mpwa wangu alikuwa anafanya kazi hapa."




**"Sina ugomvi na wewe mzee, na wala serikali haina matatizo na wewe. Jibu ambalo nitakuuliza na ambalo unalifahamu tu basi. La sivyo na wewe utafunguliwa mashtaka."**

"Ndiyo." Eddy kama ilivyo kawaida yake, alilitazama eneo lile kipelelezi.

Alipochungulia ndani aliona magari mawili yakiwa yamepaki. Moja jeupe na lingine rangi ya bluu. Hakubahatika kunakili namba, lakini kwa ujanja wa hali ya juu, alifanikiwa kupiga picha eneo hilo, lilionyesha taswira yote ya geti, magari pamoja na bustani. Aliona huenda ikamsaidia baadaye. Gari la rangi ya bluu lilikuwa aina ya Toyota Harrier la rangi nyeupe lilikuwa Toyota Alphard.

Picha zote tatu zilionyesha gari ni hilo hilo ina maana kijana aliyechukua dawa kutoka kwa Tina ama anakaa kwenye nyumba hiyo au huwa anakuja hapo kwa kufahamiana na familia hiyo, au wana undugu.

Baada ya upelelezi na vielelezo kadhaa, upande wa utetezi umegundua kuwa Abdallah Mtola awali wakati wa marehemu Chilambo alikuwa akija mara moja moja kusalimia, lakini baada ya kifo chake, anaonekana amehamia kabisa hapo.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa si mara nyingi sana Tina kuondoka nyumbani hapo na huondoka kwa nadra sana na hata kutumwa na mabosi wake, yaani baba na mama ilikuwa mara chache sana.

Mara nyingi wanaotumwa safari za nje, kwenda madukani, sokoni wakati mwingine ni hausiboi au mlinzi wa getini. Siku hiyo kulikuwa na mlinzi tu, hausiboi alikuwa amepata udhuru, alisafiri kwenda kwao. Kwa hiyo aliyetumwa kwenda kununua dawa ni Tina.

Pia mahakama iliambiwa kuwa hakutumwa na mtu yoyote yule, aliondoka mwenyewe tu jambo ambalo kwa mujibu wa upelelezi, si kweli.

Upande wa utetezi umeleta ushahidi na vielelezo kuwa ni kweli kabisa haikuwa kawaida, lakini jambo hilo siku hiyo lilifanywa kwa makusudi. Ni kwamba hausiboi hakupata udhuru kama ilivyoambiwa mahakama awali, bali aliondolewa kwa makusudi kimkakati.

Ilielezwa upande wa mashtaka kuwa siku ya tukio, mke wa Chilambo, Bi Hellen tangu saa nne asubuhi alikuwa ameondoka nyumbani hapo na watoto wake wawili, Prisca na Paul, akiwapeleka kwa shangazi yao Temeke.

Siku hiyo hiyo jioni yake, Hellen Chilambo alikuwa amealikwa kwenye sherehe za harusi zilizofanyika kwenye hoteli moja Sinza, Dar es Salaam.

Kwa maana hiyo, kuanzia saa nne asubuhi, hakuwepo nyumbani hadi alipopata taarifa za kufariki kwa mumewe akiwa kwenye harusi.

Upelelezi uliofanywa na ushahidi wake kuwasilishwa mahakamani pamoja na vielelezo navyo vinaonyesha kuwa si kweli.

Ushahidi na vielelezo vilivyotumiwa hapo ni upelelezi uliofanywa na Eddy Kamal siku aliyokwenda Goba kumfuata mlinzi wa nyumba hiyo, mzee Kalango.

"Sina ugomvi na wewe mzee, na wala serikali haina matatizo na wewe. Jibu ambalo nitakuuliza na ambalo unalifahamu tu basi. La sivyo na wewe utafunguliwa mashtaka."

Mshangao na woga mkubwa ulimpata mzee Kalango. Usiogope mzee, sema tu unayoyajua na kujibu maswali yangu kwa ufasaha, basi." Ni maneno aliyoyasema Eddy siku hiyo alipofika nyumbani kwake Goba.

"Sawa kijana nitajibu yote." Alijibu kwa hofu.

Mzee Kalango alimwambia Eddy kuwa siku chache baada ya kifo hicho aliachishwa kazi, lakini alipewa pesa nyingi ambazo zilimwezesha kujenga kibanda chake pale Goba, lakini kwa sharti la kutomwambia mtu kitu chochote. Ni siri iliyojificha.

Mzee Kalango akasema, Tina Kauzeni aliamka na kufanya kazi zake kama ilivyo siku zote. Ilipofika saa tano asubuhi aliondoka nyumbani hapo. Alirejea baada ya saa moja. Ilipofika saa nane aliondoka tena nyumbani hapo kwa tajiri yake.

Alimwambia Eddy kuwa nusu saa tu baada ya kuondoka, mke wa marehemu, Bi Hellen alirejea nyumbani hapo na ni yeye pekee ndiye aliyemuona.

"Si kweli kwamba alipopeleka watoto wake Temeke kwa shangazi yake hakurejea tena akaenda moja kwa moja kwenye harusi Sinza, alirudi saa tano na nusu asubuhi, akaniambia amerudi mara moja, lakini nisimwambie mtu yoyote yule kama amerudi, si Tina wala mumewe akirejea, lakini hakuniambia wala mimi sikujua kwa nini.

"Baadaye likatokea tukio hilo, mimi nikaona naitwa napewa pesa nyingi tu na naambiwa kazi basi, lakini nisiseme kitu chochote kuhusu siku hiyo." Mzee Kalango alimwambia Eddy siku hiyo alipomtembelea Goba.

Akaongeza kuwa mke alionekana amejifungia ndani na hata Tina aliporejea hakujua chochote kama tajiri yake amerudi na inaonekana alikuwa amejifungia chumbani kwa kufunga na ufunguo kwa ndani na Tina asingejua chochote, kwani alijua hayupo na chumba kilikuwa kimefungwa. Asingekuja kama kuna mtu ndani.

ITAENDELEA JUMAPILI



# MSIKIE JINSI ROSA REE YANAVYOMTOKA

RAPA wa kike mwenye vituko vingi, Rosa Ree, ameibuka na kusema anaamini katika Afrika hakuna mwanamuziki wa aina hiyo anayeweza kumfikia kwa sasa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Rosa Ree, amesema kwa ujumla anawaheshimu wanamuziki wenzake na kusikiliza nyimbo zao, lakini bado hawawezi kuwa kama yeye.

"Hakuna rapa ambaye ananizidi Afrika nzima. Nawapenda, nawaheshimu na nasikiliza miziki yenu, lakini mimi ndiye bora, sio wa kike, bali wote kwa ujumla," ameandika.

# Elias ainuka na jambo jipya

MWIMBAJI anayekuja kwa kasi katika muziki wa Injili, , Elias Jacob, amewashukuru mashabiki kwa mapokezi ya wimbo wake, Amen.

Elias ameliambia Nipashe kuwa amepokea shuhuda nyingi kutoka kwa mashabiki jambo linalompa faraja ya kuendelea kufanya kazi ya Mungu.

"Nashukuru kwa malezi mazuri na najisikia faraja sana kutumika chini ya Askofu Paul Sosela wa kanisa la Yesu lililopo Ushirombo, Geita," amesema.

Amesema kwenye wimbo huo amekuwa msaada mkubwa kwake na kuongeza kwamba video tayari ipo kwenye channel yake ya YouTube.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BALAA QATAR 2022

**Misri, Tunisia, Algeria zatanguliza mguu mmoja, Morocco na DRC nguvu sawa, Senegal, Cameroon, Mali hatihati...**

**KUMASI, GHANA**

WAPINZANI wakali wa soka kutoka Afrika Magharibi, Ghana na Nigeria walitoka suluhu katika mechi yao ya kwanza ya mchujo wa kufuzu Kombe la Dunia baadae mwaka huu nchini Qatar, kwenye Uwanja wa Baba Yara Sports, Ijumaa usiku.

The Black Stars (Ghana) na Super Eagles (Nigeria) walikamiana vilivyo kwenye mchezo huo uliokuwa mkali pale jijini Kumasi, wakifanya mechi yao ya marudiano itakayoamua mshindi wa kufuzu Qatar kuonekana kuwa ngumu zaidi itakapopigwa nchini Nigeria katikati ya wiki ijayo.

Ghana ilianza kwa mashambulizi ya haraka mapema kwenye uwanja wao wa nyumbani uliojaa mashabiki ambapo walijaribu kutumia kasi ya Abdul Fatawu Issahaku, Felix Afena-Gyan na Mohammed Kudus kujaribu kuipita n safu ya ulinzi ya Nigeria.

Washambuliaji wa Nigeria, Kelechi Iheanacho na Victor Osimhen nao walijaribu kusukumiza mashambulizi mbele katika robo ya kwanza ya mchezo huo, huku wakiwa na nafasi moja pekee wakati beki wa kushoto, Sanusi Zaidu alipopiga krosi iliyopaa nje.

Mchezaji Francis Uzoho wa Nigeria katika dakika ya 33 aliachia shuti kali kutoka nje kidogo ya eneo la hatari, huku pia Issahaku akijibu shambulizi kama hilo.

Super Eagles walifanya mashambulizi katika dakika za mwisho za kipindi cha kwanza, huku nafasi yao nzuri akiipata Joe Aribo alipoukimbilia mpira ulioelekezwa upande wa kulia wa eneo la hatari, lakini kiungo huyo wa Rangers akapiga shuti kali lililokwenda nje.

Dakika ya 55 mlinda mlango wa Black Stars, Joe Wollacat aliokoa shuti kali kutoka kwa Moses Simon baada ya winga huyo kuchomoka kutoka upande wa kushoto na kuuwahi mpira ambapo shuti lake liliokolewa.

The Super Eagles walipata penalti zikiwa zimesalia dakika 15, lakini VAR ilimsadia mwamuzi, Redouane Jiyed na kwamba haikuwa halali.

Nigeria na Ghana zitakutana tena kwa mechi ya marudiano mjini Abuja jioni ya Jumanne Machi 29 ambapo mshindi wa mchezo huo ndio atafuzu kwenda kombe la Dunia.

Mechi nyingine za kufuzu kwa mchujo huo zilikuwa ni Misri dhidi ya Senegal ambapo walishinda bao 1-0, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) ilitoka sare ya kufunga bao 1-1 na Morocco, Algeria iliifunga Cameroon 1-0 na Mali ikafungwa bao 1-0 na Tunisia.

## KWA UFUPI

**SALAH ATAKIWA BARCA**

KOCHA wa Barcelona, Xavi anamtaka mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29 pale Nou Camp, wakati magwiji hao wa Katalunya wakionekana kumkosa Erling Braut Haaland ambaye ndio chaguo lao kubwa. ***(Mundo Deportivo)***

**HAALAND NA BARCA**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesema hataiweka klabu hiyo kwenye hatari na mgogoro wa kifedha kwa kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21 kutoka Borussia Dortmund. ***(Fabrizio Romano, via Mundo Deportivo)***

**LEEDS HAIMUACHII RAPHINHA**

LEEDS United imeripotiwa kukataa ofa ya pauni milioni 29 kutoka Barcelona kwa ajili ya winga wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, ambaye kipengele cha mkataba wake kinamruhusu kuuzwa kwa pauni milioni 60. ***(Sport)***

**NETO AWANIWA PSG**

WINGA wa Wolves na Ureno, Pedro Neto yuko kwenye orodha ya wachezaji wanaowaniwa na Paris St-Germain wakati huu nyota huyo mwenye miaka 22 akirejea kutoka majeruhi ya muda mrefu. ***(Mail)***

**BOTMAN NA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle inajiandaa kuipiku AC Milan katika mbio za kumsajili mlinzi wa kati, Sven Botman mwenye umri wa miaka 22 kutoka Lille, baada ya kushindwa kumsajili Januari. ***(The Times)***

**NUNEZ AWINDWA**

NEWCASTLE inatazamiwa pia kuongeza nguvu kwenye safu yake ya ushambuliaji kwa kumsajili mshambuliaji wa Benfica na Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, licha ya Arsenal pia kumtaka. ***(The Athletic)***

**AKANJI AWANIWA MAN**

KLABU ya Manchester United inamtaka mlinzi wa Uswisi, Manuel Akanji mwenye umri wa miaka 26, ambaye amekataa kusaini mkataba mpya pale Borussia Dortmund na amewekewa thamani ya pauni milioni 25 na klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga. (Mirror)

**WILSON AGOMBEWA**

LIVERPOOL, Manchester City na Manchester United zinapambana kumsajili mshambuliaji kinda wa Rangers raia wa Scotland, Rory Wilson. (Star)

**UGOCHUKWU ATAKIWA EPL**

ARSENAL na Tottenham zinamtaka kiungo mfaransa, Lesley Ugochukwu mwenye umri wa miaka 18 kutoka Rennes ya Ligue 1 ya Ufaransa. ***(l'Equipe)***

**MOURINHO AMTAKA XHAKA**

KIUNGO wa Arsenal na Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 29 bado anatakiwa na kocha, Roma Jose Mourinho. ***(Gazzetta dello Sport)***

**MILENKOVIC HUYO WEST HAM**

KLABU ya West Ham itamsajili nyota walioku wakimuwania kwa muda mrefu, Nikola Milenkovic mwenye umri wa miaka 24, huku ripoti zikisema mlinzi huyo wa Fiorentina na Serbia ameingia makubaliano ya awali na wagonga nyundo hao wa London. ***(TeamTalk)***

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
ALMERIA
VERSUS
GIRONA
1 | 2.12
X | 3.32
2 | 3.27

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI ADOKEZA KUSTAAFU ARGENTINA



**BUENOS AIRES, Argentina**

LIONEL Messi atatathmini upya mustakabali wake wa kuendelea kuicheza timu ya taifa ya Argentina baada ya Kombe la Dunia nchini Qatar baadaye mwaka huu, na hajaondoa uwezekano wa kustaafu.

Messi alikuwa miongoni mwa wafungaji Ijumaa wakati Argentina ambayo tayari imefuzu ilipoifunga Venezuela 3-0 katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia kwenye Uwanja wa La Bombonera mjini Buenos Aires.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 aliiongoza Argentina kunyakua ubingwa wa Copa America mwaka jana, ikiwa ni mara ya kwanza kwa taifa hilo tangu mwaka 1993.

Argentina haijashinda Kombe la Dunia tangu Diego Maradona alipoiongoza kutwaa ubingwa huo mwaka 1986, huku Messi akikaribia zaidi mwaka 2014 walipotinga fainali nchini Brazil.

Messi, ambaye alijiunga na Paris Saint-Germain kutoka Barcelona Agosti mwaka jana, alikiri kwamba mustakabali wake wa kucheza kimataifa zaidi ya Qatar ulikuwa akilini mwake.

"Sijui nitafanya nini baada ya Kombe la Dunia. Ninafikiria kuhusu kile kitakachokuja," Messi aliwaambia wanahabari baada ya ushindi wa Venezuela.

"Baada ya Qatar nitalazimika kutathmini upya mambo mengi."

Aliongeza: "Sijui (kuhusu kucheza), ukweli ni kwamba sijui. Ninafikiria juu ya kile kitakachofuata, fikiria tu kukabiliana na Ecuador (Jumanne). Mechi za maandalizi Juni na Septemba.

"Hebu tumaini haya yatapita njia bora zaidi. Lakini kwa hakika baada ya Kombe la Dunia mambo mengi yatabadilika."

Messi aliongeza kuwa kunyanyua taji lake kuu la kwanza akiwa na Argentina mwaka jana kwenye Copa hakutaathiri uamuzi wake.

"Imepita muda kwamba nina furaha hapa, tangu kabla ya kushinda Copa," alisema. "Ninashukuru kwa haya yote wanafanya nijisikie kila ninapokuja Argentina."

Bao la nyota huyo wa PSG dhidi ya Venezuela liliendeleza rekodi nzuri ya Argentina ya kutowahi kupoteza katika kipindi cha miaka 12 wakati Messi amefunga.

Messi ameiwakilisha Argentina mara 159, baada ya kucheza kwa mara ya kwanza mwaka 2005, akifunga mabao 81.

# Ibrahimovic: Nitacheza hadi nione mtu bora kuliko mimi

**STOCKLOHM, Sweden**

ZLATAN Ibrahimovic amesema atafikiria kustaafu wakati tu kutakapotokea mtu bora kuchukua nafasi yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 40 alilireja Ulaya kwa kujiunga na AC Milan kutoka LA Galaxy ya nchini Marekani Januari 2020, akifunga mabao 33 katika mechi 55 za Serie A tangu wakati huo.

Mabao 20 kati ya hayo yalikuja mwaka 2020 pekee.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Sweden amesema anataka kucheza kadri awezavyo, hata hivyo, jambo linalomaanisha kuendelea hadi mchezaji mwingine anayestahili kuchaguliwa mbele yake.

"Wakati ujao bado haujaandikwa. Sijapanga. Wacha tuone kitakachotokea," alisema Ibrahimovic akiiambia UEFA.com.

"Sitaki kujutia kuacha soka kisha kusema kwamba naweza kuendelea kucheza soka, kwa sababu ningejutia maisha yangu yote, nikiona ningeweza kuendelea.

"Nataka kucheza kadri niwezavyo. Ukweli ni kwamba nitacheza hadi nione kuna mtu bora kuliko mimi, kwa hiyo bado nacheza."

Licha ya kutocheza mechi 18 msimu huu, Ibrahimovic ndiye mfungaji bora wa Milan pamoja na Rafael Leao na Olivier Giroud mwenye mabao nane.



## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 27/03/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 1348 | Pescara Calcio vs Pontedera | 1.66 | 3.63 | 5.18 |
| 15:30 | 1535 | Foggia vs Campobasso Calcio | 1.87 | 3.60 | 3.90 |
| 15:30 | 2143 | Nuova Monterosi vs Vibonese Calcio | 1.55 | 3.89 | 5.99 |
| 15:30 | 2619 | Fermana FC vs Cesena | 3.71 | 3.16 | 2.07 |
| 15:30 | 2964 | Carrarese vs Vis Pesaro | 2.12 | 3.24 | 3.44 |
| 15:30 | 3075 | Messina FC vs Latina | 2.27 | 3.20 | 3.15 |
| 15:30 | 3374 | AZ Picerno vs Avellino | 3.70 | 3.15 | 2.07 |
| 15:30 | 3559 | Juve Stabia vs Catanzaro | 3.74 | 3.19 | 2.04 |
| 15:30 | 3611 | Olbia Calcio vs Teramo | 2.46 | 3.14 | 2.89 |
| 15:30 | 3763 | Monopoli vs Potenza SC | 1.47 | 4.01 | 7.02 |
| 15:30 | 4322 | Maastricht vs Almere City | 4.83 | 4.04 | 1.59 |
| 15:30 | 5305 | Paganese vs Palermo | 3.46 | 3.36 | 2.07 |
| 16:00 | 4001 | FK Stechovice vs Banik Sokolov | 1.55 | 4.29 | 4.49 |
| 16:00 | 5040 | Mlks Wissa Szczuczyn vs KS Ursus Warszawa | 3.59 | 3.74 | 1.81 |
| 16:15 | 2831 | Radunia Stezyca vs ZKS Stal Rzeszow | 3.60 | 3.60 | 1.84 |
| 16:30 | 4613 | Thisted FC vs Middelfart | 1.64 | 3.75 | 4.48 |
| 17:00 | 5129 | Burgos vs Tenerife | 3.12 | 2.92 | 2.40 |
| 17:45 | 2751 | Emmen vs Telstar | 1.42 | 4.53 | 6.30 |
| 18:00 | 1404 | CF Salmantino vs CD Artistico Navalcarnero | 2.88 | 2.93 | 2.43 |
| 18:00 | 1756 | Aguilas CF vs Levante B | 2.42 | 2.96 | 2.87 |
| 18:00 | 2030 | Real Murcia vs CF La Nucia | 2.54 | 2.88 | 2.78 |
| 18:00 | 2941 | Terrassa FC vs CD Teruel | 2.48 | 3.02 | 2.73 |
| 18:00 | 3121 | SD Compostela vs Coruxo | 2.32 | 3.01 | 2.96 |
| 18:00 | 3269 | Alcoyano vs Villarreal B | 2.78 | 3.26 | 2.31 |
| 18:00 | 3578 | Naxara CD vs Real Sociedad C | 2.87 | 3.02 | 2.38 |
| 18:00 | 5464 | UP Langreo vs Arosa SC | 1.92 | 3.31 | 3.61 |
| 18:15 | 1461 | CD San Roque vs CP Cacereno | 2.43 | 3.11 | 2.72 |
| 18:30 | 2386 | AC Reggiana vs Imolese Calcio | 1.26 | 5.40 | 11.00 |
| 18:30 | 3227 | AC Siena vs Lucchese | 2.04 | 3.15 | 3.80 |
| 18:30 | 4211 | Aquila 1902 Montevarchi vs Grosseto | 1.96 | 3.39 | 3.79 |
| 18:30 | 4995 | Toledo vs Socuellamos | 2.32 | 3.01 | 2.96 |
| 18:30 | 5190 | Gubbio vs Viterbo Calcio | 1.83 | 3.45 | 4.30 |
| 18:30 | 5229 | Bari vs Fidelis Andria | 1.27 | 5.20 | 11.01 |
| 19:00 | 2054 | Ruch Chorzow vs KKS 1925 Kalisz | 1.88 | 3.45 | 3.60 |
| 19:00 | 4025 | Calvo Sotelo Puertollano vs CF Intercity | 2.87 | 2.97 | 2.41 |
| 19:00 | 5330 | Sestao vs Racing Santander B | 1.79 | 3.26 | 4.28 |
| 19:00 | 5913 | Real Betis B vs Barcelona B | 3.26 | 3.31 | 2.04 |
| 19:00 | 5944 | CD Coria vs Velez CF | 2.37 | 3.13 | 2.78 |
| 19:15 | 3351 | Malaga vs Huesca | 2.59 | 2.93 | 2.84 |
| 19:15 | 5953 | Alcorcon vs Valladolid | 4.05 | 3.46 | 1.84 |
| 19:45 | 2613 | SC Kfar Qasem vs El Fahem | 2.14 | 3.30 | 3.35 |
| 20:00 | 4337 | Pontevedra vs AD Union Adarve | 1.92 | 3.27 | 3.66 |
| 21:30 | 2494 | Sacachispas FC vs Mitre SdE | 2.41 | 2.72 | 3.16 |
| 22:00 | 5411 | Univ de Chile vs Union Espanola | 2.63 | 3.22 | 2.44 |
| 22:00 | 5433 | Almeria vs Girona | 2.12 | 3.32 | 3.27 |
| 22:40 | 2328 | Gimnasia Mendoza vs Belgrano Cordoba | 2.59 | 2.88 | 2.73 |
| 23:00 | 3255 | Portland Timbers vs Orlando City | 1.91 | 3.54 | 3.94 |
| 23:05 | 1985 | Canada vs Jamaica | 1.28 | 4.86 | 8.74 |
| 23:10 | 3339 | Deportivo Cali vs Club Cortulua | 1.65 | 3.46 | 4.88 |
| 23:30 | 3678 | San Martin SJ vs Gimnasia Jujuy | 2.01 | 2.96 | 3.78 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# REDONDO: NITASTAAFU NA RONALDO, MESSI

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji mkongwe wa klabu ya Biashara United, Ramadhani Chombo 'Redondo' amesema kuwa hatostaafu kucheza soka, mpaka wachezaji Cristiano Ronaldo wa Manchester United na Lionel Messi wa PSG waache kucheza soka.

Redondo ambaye ana zaidi ya miaka 20 sasa kwenye soka la ushindani amesema kuwa wachezaji hao ndiyo 'mashujaa' wake na wakati akianza kucheza Ligi Kuu, hao ndiyo walikuwa wanavuma, na alikuwa akiwaangalia na kuiga vitu kutoka kwao, hivyo hawezi kutundika daruga kabla ya wachezaji hao kustaafu.

"Mimi wakati naanza kucheza Ligi Kuu, jamaa hao ndiyo walikuwa vijana sana na walikuwa kwenye viwango vya hali ya juu, na mimi nilikuwa nawakubali na nawapenda sana, niliiga vitu mbalimbali kutoka kwao, leo hii eti nistaafu wakati wao bado, hapana, nasubiri wao kwanza waache kucheza soka na mimi ndiyo nitastaafu," alisema Redondo.

Kiungo huyo mwenye uwezo mkubwa wa kucheza mpira kiasi cha mashabiki wake kumpachika jina la kiungo fundi wa zamani wa Kiargentina, akichezea klabu mbalimbali, ikiwemo Real Madrid, Fernando Redondo, alianza soka la ushindani kwenye klabu ya Ashanti, kabla ya kujinga na Simba 2010, na baadaye kutimkia Azam FC mwishoni mwa msimu ambapo alikaa hadi 2012, aliporejea tena Simba hadi mwishoni mwa msimu 2014 alipohamia Villa Squad.

Alizichezea pia klabu za Mbeya City, Friends Rangers na African Lyon, kabla ya kujiunga na Biashara United 2019.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Rashid Mfaume (kushoto), akimkabidhi Tuzo mshindi wa kwanza katika mashindano ya fainali ya kuimba Qaswida za kuhamasisha wananchi kuchanja chanjo ya Uviko 19, Hamis Abdallah, baada ya kuibuka mshindi. Katikati ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana wa Kiislam Bakwata, Muaharami Pembe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Arusha,Tanga watambiana City Marathon

**Na Cheji Bakari, Tanga**

WAKATI leo Jumapili ndio siku ya Mashindano ya Riadha ya Tanga City Marathon Season 6, washiriki kutoka mkoani Tanga na wale wa Arusha wametambiana kuibuka na ubingwa wa mbio hizo.

Jumla ya washiriki 1500 wakiwemo Wakuu wa Wilaya kutoka mikoa sita nchini wanashiriki mbio hizo.

Wakizungumza na gazeti hili washiriki kutoka mkoani Tanga wamesema mashindano ya msimu huu hawatakubali tena washiriki kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Dar es Salaam na Manyara kuondoka na zawadi nono.


Wakati washiriki kutoka Arusha nao wakipania kuendelea kuweka rekodi za ubingwa.

"Sisi Tanga mwaka huu lazima tuondoke na ubingwa iwe wanawake au wamaume," alisema Hassan Issa mshiriki wa mbio za kilometa 10, huku mshiriki kutoka klabu ya JKT Arusha ambaye hakutaka kutaja jina lake akisema lazima waendeleze rekodi yao tena.

Tangu kuanza kwa mbio hizo mkoani Tanga mwaka 2017, washiriki kutoka klabu za Polisi, JKT za Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro wamekuwa wakiibuka na ushindi wa mbio za kilometa 21 na 10, wakati washiriki kutoka Tanga wanaambulia nafasi za tatu hadi tano.

Katika mbio hizo za mwaka huu za kilometa 21, 10 na 5 ambazo zitazinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, zitaanzia katika viwanja vya jumba la Makumbusho maarufu Tanga Urithi na kuzunguka mitaa ya jiji hilo na kuhitimishwa katika viwanja hivyo hivyo.

# Michezo
Jumapili Machi 27, 2022
Nipashe

## Messi adokeza kustaafu Argentina

HABARI UK 22



Nahodha wa Misri, Mohamed Salah (kushoto) akichuana na mlinzi wa Senegal, Saliou Ciss wakati wa mchezo baina ya timu hizo mbili wa mchujo wa kufuzu kombe la Dunia nchini Qatar, juzi Ijumaa. Misri ilishinda bao 1-0 la kujifunga la Ciss dakika ya 39 kwenye uwanja wa Cairo. **PICHA MTANDANO**

# YANGA SC, AZAM FC ZATOLEANA MAPOVU

## ●●● Zaka Zakazi asema Mayele ni wa kawaida hawamwogopi, Bumbuli amjibu wao wanakwenda kuchukua pointi tatu...

**Na Adam Fungamwango**

KUELEKEA kwenye mechi ya raundi ya 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Azam FC dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Azam Complex, Aprili 6, klabu hizo zimeanza kuvutana, kila moja ikitamba kushinda na kumuonya mwenzake.

Wakati Ofisa Habari wa Azam, Thabit Zacharia akisema kuwa straika anayetegemewa na Yanga hivi sasa, Fiston Mayele ni wa kawaida sana, Hassan Bumbuli amesema wanakwenda Chamazi na kuchukua pointi tatu, huku wakiutawala uwanja kwa wachezaji, mashabiki na viongozi pia dhidi ya wenzao ambao watakuwa kama wapo ugenini.

"Mechi yetu na Yanga itakuwa nzuri sana na wengi wanazungumzia kumkaba au kumzuia Mayele, yule ni straika wa kawaida tu kama wengine, ila ni kwa sababu anacheza kwenye klabu yenye mashabiki wengi kwa hiyo wanamzungumza sana. Na wakati wengi wanamzungumza, kuna klabu zingine nazo zinapambana kuhakikisha hazungumzwi sana, kumbe ndiyo wanajikuta wanamzungumzia sana," alisema Thabit ambaye ni maarufu kama Zaka Zakazi.

Alisema wakati mchezaji huyo ana idadi ya mabao 10, tayari kuna straika Mtanzania Reliats Lusajo alikuwa nayo, ila ni kwa sababu yeye hazungumzwi sana.

"Sisi Azam tumekutana na mastraika hatari zaidi, tumekutana na Ramadhani Sobi wa Pyramids ambaye alinunuliwa kutoka Ligi Kuu ya England kwa hiyo sioni cha ajabu sana, ila sema tena masikini akipata," alisema Ofisa Habari huyo.

Akijibu mapigo, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema hakatai kuwa Mayele ni mchezaji wa kawaida kwa sababu hana mapembe, wala miguu mitatu, lakini watakwenda kuchukua pointi tatu ugenini pale pale Chamazi.

"Ni kweli Fiston Mayele ni mchezaji wa kawaida, hana mapembe, wala miguu mitatu. Amesema sahihi. Ni wa kawaida kama mchezaji mwingine yoyote, lakini tutakapokwenda kucheza Chamazi, watakaojaa ni mashabiki wa Yanga. Siku zote huwa hivyo, mashabiki wa Azam hawaonekani, haina mashabiki, hata mashabiki wao ni wao kwa sababu wamelazimika, lakini kabla ya kuwa timu hiyo wameshawahi kuwa na timu zao. Na ukweli ndiyo huo, watatoe Tegeta sijui wapi, sisi wanakuja wenyewe. Tutaujaza uwanja mashabiki tutakuwa wengi kuliko wao, na hata viongozi wetu watakuwa wengi kuliko wao, na wachezaji watatawala uwanjani kuliko wao na tutapata ushindi nyumbani kwao hapo hapo," alisema Bumbuli.

# Pablo atoa maagizo kwa wachezaji

**Na Dennis Fussi**

KUELEKEA mchezo wa Simba dhidi ya US Gendarmarie Aprili 3 mwaka huu, kocha Pablo Franco ametoa maagizo mapya kwa wachezaji wake ili kuhakikisha wanapata pointi zote tatu.

Na sasa Pablo amewataka wachezaji wake kuzingatia anachowaelekeza mazoezini sababu ndio njia pekee itakayowapa ushindi katika mchezo huo Kombe la Shirikisho Afrika.

Kocha huyo amesema mbali na kuzingatia mbinu hizo, lakini pia wachezaji wake wanapaswa kutowadharau wapinzani wao sababu siyo timu dhaifu kama watu wanavyoichukulia.

**"Huu ni mchezo muhimu kwetu na ni lazima tushinde kama kweli tu nataka kuendelea mbele kwenye michuano hii," alisema Pablo.**

"Wachezaji wangu wanapaswa kutowadharau Gendarmarie hata kama tunacheza nyumbani, kwenye soka chochote kinaweza kutokea."

Simba iliyopo nafasi ya tatu kwenye kundi D, ikiwa na pointi saba sawa na RS Berkane iliyopo nafasi ya pili, inahitaji kushinda mchezo huo ili kufikisha pointi 10 ambazo zitawavusha kucheza hatua ya robo fainali.





9 770856 541002
GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042